# MWANA WA MUNGU NI NANI?

## ILI NIPATE KUMSUJUDU!

## YALIYOMO


**Tumaini lenye utukufu** ………………………………………………………… 3

**Kizazi cha wana kinachipuka** …………………………………………… 8

**Kupokezana utume** …………………………………………………………….. 11

**Kuimarishwa katika injili** …………………………………………………… 14

**Kuchaguliwa ili Kuyajua Mapenzi Yake** ……………………………….. 18

**Kudhihirishwa kwa Jina** ……………………………………………………….. 25

**Kuoshwa katika utume** ………………………………………………………… 35

# TUMAINI LENYE UTUKUFU

## Huduma ya unabii

***"Tena Yuda na Sila, kwa kuwa wao wenyewe ni manabii, wakawausia ndugu kwa maneno mengi, wakawathibitisha"* Mdo 15:32.** Huduma ya kinabii **huinua** na **kuthibitisha** kwa maneno mengi. Lakini maneno haya mengi yaliyotumiwa na hawa manabii yalikuwa yapi? Wengi wa wanaoitwa manabii kanisani wametumia maneno mengi lakini hawakuweza hakika **kuwausia** na **kuthibitisha** wandugu katika mapenzi na kusudi la Mungu kulingana na neno lake. Mungu anataka tupokee neema inayopatianwa kupitia huduma ya nabii ili tuweze kujengwa kuwa mwili uliokomaa wa Kristo (**Efe 4:7-16)**. Twapaswa kuwa na ufahamu zaidi kuhusu wajibu wa manabii na maneno ambayo wanastahili kutumia.

## Kupatiana matumaini ya uongo

Katika siku za Yeremia, wengi waliojiita manabii walinena katika jina la BWANA ("MIMI NDIMI"). Hata hivyo Yeremia aliwaomboleza, na Mungu akanena kuwahusu, ***"Hunena maono ya mioyo yao wenyewe, hayakutoka katika kinywa cha BWANA. Daima huwaambia wao wanaonidharau, BWANA amesema, 'mtakuwa na amani' nao humwambia kila mtu aendaye kwa ukaidi wa moyo wake, 'hamtapatwa na ubaya wo wote'. Mimi sikuwatuma manabii hao, lakini walikwenda mbio; sikusema nao, lakini walitabiri"* Yeremia 23:16-117, 21.**

Wengi leo wangenena katika jina la Yesu kwa watu wa Mungu lakini ujumbe ni upi? "Manabii" hawa katika wakati wa Yeremia walikuwa wakiwahimiza wandugu katika uasi wao kwa Mungu, wakitabiri kutoka kwa mioyo yao, bila kupeana neno la Bwana. Walikuwa wakipatiana tumaini la uongo kwa watu badala ya kufunua tumaini ambalo hutoka na liko ndani ya Yesu!

## Kujenga Ukuta

Mungu alisema kupitia Ezekieli ***"Tabiri juu ya manabii wa Israeli wanaotabiri, uwaambie wanaotabiri kwa mioyo yao wenyewe, Lisikieni neno la BWANA…Hamkupanda kwenda mahali palipobomolewa, wala hamkuitengenezea nyumba ya Israeli boma, wapate kusimama vitani katika siku ya BWANA. Wameona ubatili, na uganga wa uongo, hao wasemao, BWANA asema; lakini BWANA hakuwatuma; nao wamewatumainisha watu ya kuwa neno lile litatimizwa"* Ezekieli 13:2,5-6.**

Watu hawa hawakuwa wakiwathibitisha wandugu wala hawakuwa wakifunika mianya katika ukuta. Wakati Petro alimwona Yesu akibadirishwa alisema ilithibitisha lile neno la unabii la maandiko (**2 Petro 1:19-21).** Watu hawa hawakuwa wamesikia kutoka kwa Mungu; kwa hivyo, hawakuwa na uhakika kwamba neno lao lingethibitishwa. Kwa hivyo, katika siku za Yeremia na Ezekieli, watu wa Mungu hawakuweza kusimama katika siku ya hukumu; hawakuweza kusimama katika vita. Walichukuliwa mateka na kuyapoteza maisha yao na tumaini lao.

## Kusimama

Huduma ya kweli ya kinabii ni kujenga ukuta wa nyumba, ili katika siku ya Bwana, nyumba inaweza kusimama. ***"Nyumba ya Mungu ni kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli"* 1Timotheo 3:15.** Nyumba ya Mungu inajengwa juu ya na katika ukweli!

Mtume Paulo alisema kwa **Waefeso** yakuwa iliwapasa kuvaa silaha zote za Mungu ili siku ya uovu wapate kusimama (**Waefeso 6:10-18**).

Silaha zote za Mungu zinaongea juu ya ukweli wa Neno la Mungu ukitufunika kikamilifu, zikilinda utu wetu na kuthibitisha msimamo wetu juu ya uongo wa yule mwovu. Mungu alisema kupitia Ezekieli ya kuwa ***"hayatakuwapo tena maono yo yote ya ubatili, wala ubashiri wa kujipendekeza, katika nyumba ya Israeli"*** **(Ezekieli 12:24).** Hapana tena unabii wa kiubinafsi ambayo inatamani mambo ya kiubinafsi; sio tena unabii unaofundisha watu kutafuta kuepuka adha; sio tena ubabii unaoahidi mambo mengi lakini hauna mazao ya kudumu. Huku ndiko kujenga ukuta na ***"chokaa usiokorogwa vyema"*** ambayo, mvua ya mawe, mafuriko makubwa ya barafu itaanguka na walio ndani yake wataangamia. (**Ezekieli 13:10-14).**

Nyumba ambayo Yesu anaijenga ina misingi na huduma ya kinabii ni moja wapo ya huduma ya kimsingi (**Efe 2:20). Manabii wanahitajika kujenga ukuta** wa nyumba ili nyumba iweze kusimama dhidi ya majaribu katika vita katika Siku ya Yesu.

## Kuzingatia hatima yetu.

Katika kitabu cha ***maombolezo*** Yeremiah anaomboleza anguko na uharibifu wa Yerusalemu na mateka katika uhamisho kule Babeli ya wakaazi wake. Anasema sababu ya anguko lake ni ***"hakukumbuka mwisho wake; kwa hiyo ameshuka kwa ajabu"*** **Omb 1:9.**

## Mji wa Mungu

Yerusalemu katika agano la kale ulikuwa ni mji ambapo Mungu alichagua kuliweka Jina Lake na uwepo. Anasema kumhusu katika **Isaya** ya kwamba Anafurahishwa ndani yake na kwamba Mungu ana furaha juu yake kama bibi harusi **(Isaiah 62:4-5).**

Lakini kuna mji ambao Ibrahimu aliuona ***"ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu"*** **Ebr 11:10.** Hii inazungumza habari ya Yerusalemu wa juu (**Wagalatia 4:26**), Yerusalemu wa mbinguni (**webrania 12:22),** Yerusalemu mpya aliyepambwa kama bibi harusi akishuka toka mbinguni (**Ufunuo 21:2-3);** inazungumza kuhusu kanisa, Bibi harusi Wake (**Waefeso 5:22-33**).

Kanisa limeoza, limeharibika na likachukuliwa mateka Babiloni- mipangilio ya dunia. Ameenda mbali kwa filosofia za ulimwengu, kanuni za kibiashara, mitindo na njia za kumfanya awe na uvuto kwa ulimwengu-ili awe na washirika wengi badala ya kuwaleta waumini katika ukomavu ndani ya Christo. **Hakuzingatia hatima yake.**

## Maono ya kinabii

**"*Pasipo maono, watu huacha kujizuia*"** **Mithali 29:18.** Kijumla hapajakua na maono ya kinabii ya kweli yaliopeanwa kanisani. Kwa hivyo, ameacha kujizuia; hajabadilishwa na neno la Mungu, hajapata utungu au uchungu katika neno kumleta mtu aliye kamilika, mtoto mwanamume atakayetawala Mataifa (**wagalatia 4:19, Ufunuo 12:5**)! Amepotoshwa na walimu wa uongo na manabii na akajiruhusu kuondolewa ***'kwa tumaini la injili'*** **(Wakolosai 1:23).**

Wakati maono ya kinabii ambayo yamepatianwa kupitia neno la Mungu yanatangazwa yataachilia mwili wa Kristo kujengeka, kufikia ukomavu na kuyakamilisha mapenzi yake. Mungu hajatuita kupungukiwa na utukufu wake; ametuita tuwe mtu mkamilifu (kwa pamoja), aliyejengeka katika cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo (**Waefeso 4:13), "*Ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa***

***utimilifu wote wa Mungu"* (Waefeso 3:18-19).** Tumeitwa ili tujazwe na utimilifu wote wa Mungu! Utimilifu wote wa Mungu tena ukikaa ndani ya mwili ulimwenguni! HO!! (**Wakolosai 2:9-10).**

## Tumaini la injili

### Imani na tumaini

Mtume Paulo anatuhimiza kuendelea katika imani, sio kuondolewa kwenye tumaini la injili ambayo ilihubiriwa **(Wakolosai 1:23).** ***"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana"* Ebr 11:1.** Katika Warumi Paulo anasema ***"Bali tukikitarajia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi"* Warumi 8:25.**

Tunatumaini katika kusudi la Mungu; mpango Wake utatimilika; matokeo Yake yatafaulu. Tunatumainia hatima ya Mungu kwetu. Imani yetu iko katika ahadi za Mungu yakwamba atatufikisha hapo. Imani inatupa uhakika wa mambo tunayoyatarajia. Imani ni sasa na iko katika neno lake kwetu ili hatima yake kwetu itimilike! Hallelujah! Tunatumaini la ajabu katika injili na tunajua litatimilika maana tunamwamini Mungu kulingana na neno lake!

### Tumaini letu ni lipi?

Tumaini ambalo wengi wetu wamelihubiri na kulishikilia ni maono yaliyoghoshiwa ya uongo. Tumehubiri tiketi ya mbinguni iliyofikiriwa; kunyakuliwa kwa kanisa kutoka kwa dhiki; nyumba kule hewani na kwa hivyo tumepatia kanisa tumaini la uongo bila neno la Mungu kuwa msingi wa imani yetu.

Wakristo wamegawanyika na wameuana kwa mambo ya kimwili kwa maana hawajaliona ***"tumaini moja la wito wetu"* Waefeso 4:4.** Wakati dhiki inapokuja, kanisa limejipata likianguka maana hatujajua tumaini "***tulio nayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia***" **(Waebrania 6:19)**

### Kufurahia katika tumaini la utukufu

Paulo anasema kwamba ***"Tunafurahia katika tumaini la utukufu wa Mungu"*** (**Warumi 5:2).** Tumaini letu ni katika utukufu! Nanga yake ni katika Kristo ambaye ni mtangulizi wetu ambaye ameingia katika utukufu (**Waebrania 6:19-20).** Yesu mtu, maisha yake na maneno yake, ndio tumaini letu. Tunatumaini ndani ya Yesu na tunaamini yeye ni Bwana na kuwa Mungu alimfufua katika wafu. Tumaini letu ni kwamba nasi tutamfuata vivyo hivyo! Tutafufuliwa kama vile Yesu. Paulo alisema ni ***"kwa ajili ya tumaini na ufufuo wa wafu"*** Iliofanya ahukumiwe na kuteswa (**Mdo 23:6**).

Tumaini letu ni katika utukufu wa Mungu! Ya kwamba anatubadilisha katika mfano wa Mwana Wake (**Warumi 8:29**); kwamba tunabadilishwa na Roho sana katika mfano wake (**2 Kor 3:18).** Tumaini letu ni ***"Atakapodhihirishwa, tutafanana Naye, kwa maana tutamuona kama alivyo"* (1 Yohana 3:2).** Ni **"*Kristo ndani yetu; tumaini la utukufu"* Wakolosai 1:27**

### Tumaini dhabiti

Hii sio imani isio na maana, isio wazi, ama yenye kufikiliwa. Ni mpango wa Mungu alioupanga; ***itatendeka!*** Imani halisi haijawekwa juu ya hadithi au 'mambo ya kisayansi' juu ya mambo ya nyakati za mwisho. Mungu hajaweka hatima yetu tuwe wahuduma wazuri, ama

wenye biashara waliofaulu, hata kama hapana jambo mbaya juu ya mambo haya; ameweka hatima yetu tufanyike kuwa wana (**Efe 1:5**), kujaza dunia na maarifa ya utukufu wake (**Habakkuki 2:14**). Twatakiwa tukamilike kama Yesu hapa duniani. Maisha yake yakikamilika kupitia mwili wake, walioitwa!

Yesu ana mwili wa Roho wake duniani! Ni kanisa lake, bibi harusi Wake. Anatakiwa awe na utukufu na akiwa amekamilika bila ila wala kunyanzi (**Efe 5:27).** "***Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo" 1 Wathesalonike 5:23.*** Mungu anaunda mwili wake mkamilifu utakayedhihirisha Jesu duniani na katika dunia.

Tumaini letu ni katika utukufu ambao utafunuliwa kupitia wana wa Mungu wakidhihirishwa na kukomboa viumbe vyote (**Warumi 8:18-19**).

## Imani hii inatuzuia

***"Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu" 1 Yohana 3:3.*** Petro, akizungumza katika matumaini ya kuja kwa yesu na waasi wote wakiteketezwa, anasema, "***Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenedo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; Ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka"*** **2 Petro 3:11-12.** Tumaini hili liko katika kuja kwake! ***"tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na mwokozi wetu"*** **Tito 2:13.**

Kuja kwa Yesu ni tumaini letu na kwa sababu ya tumaini hili tunazuiliwa, ***"Nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa"*** **Tito 2:12.** Tumaini hili lililowekwa mbele yetu latufanya kujinyenyekesha kwa nidhamu ya Mungu kwa sababu twafahamu mpango wa Baba wetu na kumruhusu kuturekebisha na kutukemea. Tunataka kupitia kila hali iwapo tu tutafikia kwa tumaini hili (**Wafilipi 3:8-14**).

## Tumaini katika dhiki

Tumaini la injili latuwezesha kustahimili dhiki kwa sababu ***"dhiki kazi yake ni kuleta saburi, na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo, kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini"*** **Warumi 5:3-4.** Wakati macho yetu yanaangaziwa ili tufahamu tumaini la mwito wake (**Efe 1:17**), inatuwezesha kustahimili na kwa subira kungoja tumaini litimilizwe. Tumaini lililotimizwa ni mpango uliokamilika na ni mti wa uzima (**mithali 13:12**).

## Unahubiri tumaini lipi?

Twahitaji kuzingatia njia zetu. Ni wakati wa kulikumbatia tumaini la injili kulingana na neno la Mungu, kujenga ukuta ambao utasimama siku ya vita, katika siku ya Bwana. Utatuzuia, na kutuweka katika lengo na kuleta kusudi la Mungu katika maisha yetu binafsi na kama mwili wake. ***"Natumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi"*** **Warumi 5:5.**

Mungu anawaita wahubiri watangaze tumaini! Kuwapatia mwili wa Kristo ono la kweli la kinabii ili aweze kujizuia kutimiza mapenzi yake. Kama tukiruhusu maono ya uongo,

tutawapatia wandugu tumaini la uongo. Wakati Petro aliona Yesu akibadirishwa katika mlima, alisema ya kuwa aliweza kuwajuza wapendwa zile ***"nguvu na kuja kwa Bwana wetu"*** na alikuwa na lile ***"neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu"*** **2 Petro 1:19.**

***Manabii wa agano jipya wanatakiwa kuhimiza na kuwatia nguvu wandugu kwa maneno sawa kuhusu tumaini. Mwili wa Kristo, zingatia hatima yako na ulitimize tumaini lililowekwa mbele yako!***

# KIZAZI CHA WANA KINAINUKA

### Kuwa na roho ile iliyokuwa na Kalebu na Yoshua

Ni wakati wa kuvingirisha aibu ya misri kutoka kwetu (**Yoshoa 5:9**). Ni wakati wa tohala ya ndani kupitia Roho (**Wafilipi 3:3, Wakolosai 2:11**); kuingia katika Roho wa kuwa mwana kama Kalebu na Yoshua (**Hesabu 14:24, 32:2**); kuendea kwenye urithi kama Elisha pamoja na Eliya (**2Wafalme 2:1- 12).** Ni wakati wa kufahamu urithi wa Masihi na kupokea urithi na kupokea ahadi zote za Mungu ambazo ni ***"ndio; tena kwa hio katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi"*** **(2Wakorintho 1:20.)**

### Mataifa ni warithi

Sisi mataifa ni warithi pamoja na watakatifu wa agano la kale na washiriki wa nyumba mwa Mungu (**Waefeso 2:19**). Sisi tuliokuwa mbali tumeletwa karibu na damu ya Yesu ambaye amevunja ukuta wa katikati ambao ulikuwa umetutenganisha (**Waefeso 2:13-18**). Sisi ni warithi pamoja na warithi wa ahadi. Kwetu sasa kuna kufanywa wana (**Warumi 9:4**) – kwa wote ambao ni wa imani ya Ibrahimu (**Wagalatia 3:6-9, 26-29**)

### Jaza ulimwengu

Utume wa adamu ulikuwa ***"kujaza nchi"*** **(Mwanzo 1:28).** Hakuambiwa achukue sehemu moja ya shamba katika katikati mwa mashariki! Alitumwa AJAZE NCHI!

Nuhu alitumwa ***"ajaze nchi"*** **(Mwanzo 9:1).** Mungu alifanya ahadi kwa Ibrahimu kumpa nchi ambayo ***"katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa"*** **(Mwanzo 12:3, 13:15).** Mungu alimwambia Musa "***Lakini hakika yangu, kama niishivyo, tena kama dunia hii nzima itakavyo jazwa na utukufu wa Bwana"*** **(Hesabu 14:21).**

### Mataifa ndio urithi

**Zaburi 2** Yatuambia kuwa Masihi, Mwana wa Mungu ana ***"Mataifa kuwa warithi wako na miisho ya dunia kuwa milki yako"*** **aya 8.**

Katika siku za Yoshua waovu waliondolewa ili wawapatie watu wa Mungu urithi wao kutoka kwa Yesu. Kwa hivyo ndivyo itakavyo kuwa katika nyakati za mwisho wa dunia: ***"Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi"*** **(Mathayo 13:36-43)**

Yesu aliwatuma mitume ***"Wakawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"*** **Mt 28:19** na kuwaleta mataifa ***"wapate kujitiisha kwa imani"*** **Warumi 1:5.** ***"Na mataifa watatembea katika nuru yake, na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake"*** **Ufu 21:24.**

***"Nyota itatokea katika Yakobo; na fimbo ya enzi itainuka Israeli"*** **Hesabu 24:17.** ***"Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda wala mfanya sheria kati ya miguu yake, hata atakapo kuja yeye SHILOH, Mwenye milki ambaye mataifa watamtii"*** (**Mwanzo 49:10**).

### YESU NI MUNGU.

***"Na bila shaka siri ya utaua ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili, Akajulikana kuwa na haki katika roho, Akaonekana na malaika, Akahubiriwa katika mataifa, Akaaminiwa katika ulimwengu, Akachukuliwa juu katika utukufu"*** **1 Timotheo 3:16.**

Masihi ni Mwana wa Mungu (**Mathayo 16:16**). Mfalme Mkuu ni Mungu katika mwili! **Neno lilifanyika mwili! Yohana 1:14.** Mungu anatawala kupitia mtu aliyemchagua: ***"Atakayo***

***wahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu Yule aliyemchagua"*** - Hata Yesu Masihi wa Nazareti – na amedhibitisha haya kwa kumfufua katika wafu! **Mdo 17:31**.

## Ufalme wa Mungu

Yesu akamjibu Pilato, ***"ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa"*** **Yohana 18:36**

Ufalme wa Mungu ni haki (ambayo inakuja kwa imani, **Wafilipi 3:9**), amani (ambayo inakuja kwa imani, **Warumi 5:1**) na furaha (ambayo ni nguvu zetu, **Nehemaya 8:10**) katika Roho Mtakatifu (**Warumi 14:17**).

***"Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme"*** **Luka 12:32.** Mungu ameahidi katika **Danieli 7** ya Kwamba ***"Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii"*** **Aya 27.** ***"Nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme"*** **aya 22.**

## Masihi alikufa kwa ajili Yetu

Lakini Mungu alionyesha upendo wake kwetu kwamba wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi Masihi alikufa kwa ajili Yetu, **Warumi 5:8**. Mkombozi wetu alikuja! (**Ruthu 2:20, 4:9:22**). Yesu, masihi, ambaye ndiye aliyekuwa mbegu ya Daudi kulingana na mwili na akadhibitisha kuwa Mwana wa Mungu kupitia kufufuka (**Warumi 1:3-4**), ni mkombozi wetu. ***"Mungu alimtuma mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana"*** **Wagalatia 4:4-5.** Yesu alikufa atufanye wana, warithi wake ambao watapokea ufalme kama urithi**.**

Mungu amekuja kuwaokoa watu wake, kuwanunua watu ambao wametengwa kwa ajili yake; watu ambao atapatia ufalme wa Mungu duniani! Watu ambao wataangalia mali yake, ambao wameubwa kwa mfano wake na sura yake **(Waefeso2:10, Warumi 2:29, 12:1-2).** Kuubwa tena huku kunafanyika maishani mwetu ***"Na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu"*** na ***"Mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sasa na mfano wake yeye aliye uumba"*** **Efe 4:23 -24, Wakolosai 3:9-10.**

## Kama tukistahimili, tutamiliki pamoja naye (2 Timitheo 2:12a)

Ni wakati wakufanya upya maagano yetu na Mungu wa Israeli ***"Hamjafanya vita hata kumwagika damu mkishindana na dhambi"*** na "***tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana"*** **Waebrania 12:4-5.** Twapaswa kustahimili urudi na kumruhusu Mungu kutushugulikia kama wana.

Ni wakati wakuinuka – ni wakati wa kunyakua nchi, ***"Ili mataifa yajazwe na mafundisho haya"*** **Mdo 5:28.** Hakuna nafasi ya kuzimia roho. Utiifu wa upendo kwa dharura unahitajika. ***"Maana mtafakarini sana aliyestahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka mkizimia mioyoni mwenu"*** **Waebrania 12:3.** Mfalme wetu alistahimili msalaba, akidharau haibu, na ameketi chini katika mkono wa kuume wa enzi ya Mungu (**Waebrania 12:2).** Twapaswa ***"kupiga mbio kwa saburi katika yale mashidano yaliyowekwa mbele yetu"*** **aya 1.**

### Pigana vita vyema vya imani

Yesu yu hai! Ni lazima tuzaliwe kutoka juu! Lazima tuwe na kule kukiri kuzuri katika midomo yetu – tukitangaza sisi ni akina nani na tumetoka wapi, hata kama vile Yesu alivyo fanya **(Yohana 18:36-19:11**). Sisi tu wana wa Mungu, warithi wa ahadi, wafalme na makuhani ambao wamepewa nafasi kuchukua nchi, kurithi nchi.

Ni wakati wa ***“Wenye haki kung’aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio, na asikie”*** **Mt 13:43.**

# KUPOKEZANA UTUME

## Uwanafunzi wa kweli unahitajika kwa mataifa

Ninapoenda katika safari za kihuduma, nikisafisi mataifa ya ng'ambo hua ninarudi nyumbani na picha nzuri katika moyo wangu na mawazo kuhusu hoja kuu ya kuwa na wanafunzi wa kweli katika mataifa. Safari za kihuduma zinatia ndani mwangu nguvu kuliko mbele hitaji hili katika mataifa, na zinaambatana, imekuwa jukumu kubwa kubaki mwaminifu katika mwito na kuwa mfano wa yale tunahubiri.

## Jinsi utume umekuwa ukiendelea kwa miaka.

Baada ya kurudi nimekuwa nikisoma kitabu, **"The pilgrim church",** na E.H Broadbent. Broadbent anafuatilia historia ya waumini wa kiutume kutoka wakati wa mitume wa kwanza. Imekuwa ya kutia moyo kuona ya kwamba hata kupitia kipindi cha historia yenye tunaita 'kipini cha giza', kulikuwa na watu ambao walikuwa wanang'aa nuru ya injili ya Kristo wakitembea katika ufunuo wa kitume wa kimaandiko.

Kikundi kimoja kama hicho kinachotajwa ni "Waldenses" ambao wana mizizi kutoka kwa mitume wa kwanza na wakaishi Alpin Valleys ya Piedmont katika France. Waamini hao hawakujipatia jina hilo, lakini walitambuana kama 'wandugu' walikuja kujua juu ya makanisa yenye mipangilio ya nyakati hizi katika karne ya **12,13,** na wengi walipoteza maisha katika hali yao ya kuwa na imani ambayo haikubariani.

Katika Karne ya **16** watawala wapya walianza kuchukua nafasi ya mahali walipoishi. Walipoulizwa tabia yao ya udini ilitoka wapi, walijibu, "*hebu mkuu wako azingatie, yakwamba dini ambayo tuko ndani yake sio tu dini ya nyakati zetu, au dini ambayo imetambulika kwa mara ya kwanza miaka michache iliyo pita wakati maadui wetu walijifanya, lakini ni dini ya baba zetu na babu zetu, ndio, ya baba zetu na waliotutangulia kwa mbali. Ni dini ya watakatifu na ya wafia dini, ya wanaokili na ya mitume"*

## Mafundisho ya kimaandiko yakizingatiwa.

Wakati wandugu hawa walikutana na wanaoleta mabadiriko katika karne ya 16 walisema, "*wazee wetu mara kwa mara wametuhesabia kwamba tumekuwako tangia siku za mitume. Katika kila hali hata hivyo, twakubaliana nanyi, na kufikilia kama ninyi, kutoka siku zile za mitume wenyewe tumefuatilisha kuheshimu imani".*

E. H. Broadbent anatuonyesha kwamba waamini hawa hawakuwa matunda ya mabadiliko "*bila kuonekana na msukumo wa kanisa hizo, zaonyesha kinyume, kuendelesha tamaduni, uliowafikia kutoka chanzo nyingine – mafundisho ya maandiko na utendaji wa kanisa lililobaki nyuma"*

Hawakuwa na kukiri spesheli kwa imani ila tu maandiko matakatifu na bila mtawala, lakini kumfuata Yesu, ndio lilikuwa lengo lao kubwa. Walitegemea Roho wa Kristo aliyedumu ndani yao kufungua ufunuo kutoka kwa maandiko, wakijitoa katika kukua kwa maarifa na ufahamu wa Neno. Walibatiza wale walioamini na mara kwa mara walishiriki chakula cha Bwana pamoja wakimkumbuka.

Katika mipangilio ya kanisa waliongozwa na wazee na wakaamini katika "kupokezana utume" kupitia kuwekewa mikono kwa wale walioitwa ili wapokee neema hiyo. Mitume hao walikuwa wakitembeatembea wakati wazee na waangalizi walikaa manyumbani mwao na kanisani. Kanisa lote walishiriki katika kusimikwa huko.

### Kila mara Mungu ana mabaki

Ni ya kuhimiza kuona kwamba kumekuwako na watu wa imani, ambao hawajaharibiwa na tabia za dunia na za kidini, kwa unyenyekevu wakitii Neno ambalo limewafikia kizazi hadi kizazi; kikundi cha watu wakiwa na maandiko yakiwa ndio chanzo cha imani na utendaji, wakifuata mfano uliowekwa na Bwana Yesu na mitume ambao amewainua. Waliendelea na imani hiyo na ***"Kuishindania imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** **Yuda 3. Twatakiwa kuwa watu kama hao!**

## Warekabu, kikundi cha kitume!

### Kutii maagizo ya baba yao

Katika siku za Yeremia, kulikuwa na jamii ambayo ilitoa jina kutoka kwa baba yao, Jonadabu, mwana wa Rekabu. Jonadabu ni mfano wa baba wa kiutume ambaye sauti yake ilizingatiwa katika vizazi, hata baada ya karne mbili. Yeremia aliambiwa na Yahwe (BWANA) awakaribishe kizazi cha Jonadabu katika nyumba ya Yahwe wanywe divai lakini hawakunywa wakisema, ***"Hatutakunywa divai; kwa maana Jonadabu mwana wa Rekabu baba yetu alituamuru, akisema, msinywe divai ninyi wala wana wenu hata milele"*** **Yeremia 35:6**

Kulikuwa na maagizo mengine yaliopatianwa na Jonadabu ambayo watu hawa wangenukuu kwa maneno kila kitu kama kilivyonenwa karne mbili tangu alipoishi. Hata katika uwepo wa nyumba ya Yahwe hawakuwa na hali ya kutotii neno la baba yao.

Jonadabu alikuwa mtu mkuu katika siku zake, akitumiwa na Mungu kuungana na Mfalme Yule mpya aliyetiwa mafuta wa Israeli, Yehu, katika kuangamiza ibada ya uongo ya siku na kuleta anguko la nyumba ya Ahabu na uharibifu wa mke muovu wa Ahabu Yezebeli (**2 Kings 10:15-17**). Mtu huyu, Yonadabu, alikuwa ameyatoa maagizo kwa watoto wake ambayo baadaye yalipitishwa kwa vizazi vyake, wakatii kwaa bibii kwamba ilimshika Mungu.

Mungu alitumia mfano wao kuhukumu na kuamua waesraeli wengine katika siku za Yeremia kwa kusema, ***"Maneno ya Yonadabu, mwana wa Rekabu aliyowaamuru wanawe, kwamba wasinywe divai, yametimizwa, na hata leo hawanywi; maana waitii hiyo amri ya baba yao; lakini mimi nimesema nanyi, nikiamka mapema na kunena, bali ninyi hamkunisikiliza mimi"*** **Yeremia 35:14.** Thawabu ya uaminifu huo ilikuwa ***"Yonadabu, mwana wa Rekabu, hatakosa kuwa na mtu wakusimama mbele zangu hata milele"*** **Yeremia 35:19**

## Kuwa sehemu ya utume

### Yesu ni Baba yetu.

Kuwa sehemu ya "utume" yamaanisha kuwa sehemu ya kikundi cha watu, kama Waldenses na Warekabu, ambao kwa uaminifu wanatembea katika kutii imani ya baba yao toka kizazi hadi kizazi. Baba wetu wa kitume ni Yesu. Yeye ndiye ***"Mtume…wa maungamo yetu"*** **Wabrania 3:1.** Yeye ndiye aliyetumwa kutoka kwa Mungu kuyanena maneno Ya Mungu, na akapewa Roho bila kipimo **Yohana 3:34**. Yeye ndiye ambaye ndani yake tuna ufunuo kamili wa Baba, kama alivyo nena na Filipo, ***"aliyeniona mimi amemwona Baba"*** **Yohana 14:9**. Moja wapo wa jina lake tulilopewa na Mungu kupitia nabii Isaya ni ***"Baba wa milele"*** **Isaya 9:6**

Kuwa sehemu ya "utume" yamaanisha kukubaliana na neno la Mungu ya kwamba Yesu ni Baba wetu wa kitume na yakwamba tutayafuata maagizo yake, kwa uaminifu tukiyafikishia vizazi bila kuraghai.

### Yesu aliwainua mitume 12 ili kuendelesha kazi ya kiutume

Kazi ya Yesu ya utume ilihusisha kuwainua mitume kumi na wawili ambao wangemuakilisha kikamilifu, ***"na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi"*** **Mathayo 28:20.** Wakati waamini wa kwanza walimjia Yesu siku ya Pentekote ***"Walidumu katika fundisho la mitume…"*** **Mdo 2:42.**

Mafundisho ya mitume ilikuwa ni mafundisho ambayo walikuwa wamepokea kutoka kwa Baba yao wa kiutume, Yesu. Mitume kwa uaminifu walipatiana neno la Yesu kwa wanafunzi wapya na matokeo yalikuwa ishara na maajabu zikifanywa na kuchipuka kwa watu wenye upendo, waaminifu, na waliojitoa. **Mdo 2:43-47**.

### Ili ulimwengu ujue ya kwamba Mungu alimtuma Yesu

Wakati Yesu alimwomba Baba usiku kabla yake kwenda msalabani alimueleza Baba kwamba ameaminika kufanya kazi ya kiutume ya kuwainua mitume kumi na wawili ambao angetuma ulimwenguni kama Baba alivyomtuma (**Yohana 17:4-19**). Kisha ***"Akawaombea wale watakao amini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja kama wewe Baba ulivyo ndani yangu nami ndani Yako; hao nao wawe ndani Yetu ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliye nituma"*** **Yohana 17:20-21**

Kuwa sehemu ya "utume" inamaanisha kuwa sehemu ya ombi hili. Inatakikana ijulikane kwamba umoja hauletwi na miungano ya umoja, mizuri kama inawezakuwa. Umoja huja wakati waume na wake wanaamini neno lililonenwa na mitume ambao walifunzwa na kuandaliwa na Yesu. Huu ni ***"umoja wa imani"*** iliyonenwa na mtume Paulo katika barua yake kwa waefeso (**Waefeso 4:13**)

Migawanyiko katika mwili wa Yesu inakuja kwa sababu watu wamejipatiana kwa dini na mashirika juu ya mafundisho ya kitume ya maandiko. Watu wakifuata mafundisho ya watu wengine na kuwa wafuata watu wanafilosophia juu yake ilileta shinda ya migawanyiko katika kanisa la Korintho ambalo Paulo aliandikia. Aliwasihi, ***"Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja"*** **1Wakorinto 1:10.** Umoja wa aina hii unawezekana tu na kanisa likiwa la "kitume", likitii maandiko, mafundisho ya Yesu na mitume.

- Ni wakati tena wa kuwapokea mitume ambao wanaleta ufunuo wa kitume na mafundisho ya maandiko.

- Ni wakati wa kuwa huru kutoka kwa mambo tuliyo jipatiana kwake na kumpokea Yesu mtume kama Baba yetu.

- Ni wakati wa kuwa sehemu ya kikundi cha kitume tukitembea pamoja na wandugu na wadada ambao wamejipatiana katika kutii neno la kitume ambalo limepatianwa kwetu katika maandiko.

- Ni kupitia ***"neema na utume"*** ambapo mataifa watatii imani (**Warumi 1:5**) na dunia itajua kwamba Mungu alimtuma Yesu!

# KUIMARISHWA KATIKA INJILI

Katika kufunga barua yake kwa Warumi, mtume Paulo anaandika tamati ambayo inatupa funguo kwa ufahamu jinsi Mungu anaweza kutuimarisha. Anaandika, ***"Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii imani…"*** **Warumi 16:25-26**

## Kuimarishwa

Ni mapenzi ya Mungu sisi tupate **"kuimarishwa".** Katika waraka wa pili wa Petro anaandika, ***"kwa hiyo nitakuwa tayari kuwakumbusha hayo siku zote, ijapokuwa mnayajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo"*** **2Petro 1:12.** Twahitaji kuimarishwa katika ***ukweli wa sasa.*** **Ukweli wa sasa** ni ukweli wa neno la Mungu likifunuliwa kwetu katika wakati huu na Roho Mtakatifu. Ni kufahamu kusudi na mapenzi ya Mungu kwa sasa ambayo yanafunguliwa kwetu katika maandiko; ni kuwa ***"macho ya mioyo yetu yatiwe nuru tujue …"*** mapenzi ya Mungu (**Efe 1:18**); ni kupokea ***"roho ya hekima na ufunuo katika kumjua yeye (Yesu)"*** **Efe 1:17.**

Twahitaji kuwa na **sikio la kusikia vile Roho anasema kwa makanisa** na kuimarishwa katika ukweli ambao ni wa sasa miongoni mwetu. Wengi wameimarisha mazingatio ya imani, dini zao, ngazi na utendaji kazi wao na wamejipatia vitambulisho katika hayo. Lakini Mungu anataka watu ambao wako tayari kuondoka na kuenenda naye – watu walioimarishwa katika ukweli wa sasa.

## Kuna mambo matano muhimu ambayo Paulo anashiriki nasi, kutuwezesha kuona vile Mungu atatuimarisha.

### 1. Kulingana na "injili Yangu"

Elewa kwamba Paulo hata hakusema ni kulingana na injili Ya Yesu, ama injili Ya Petro ama injili ya mwingine yeyote – ni ***"kulingana na injili yangu".*** Paulo alibinafsisha injili; aliipokea, aliishi na akaipumua. **Ungekutana na Paulo, umekutana na injili.**

Paulo alipowaona Petro na Baranabas wakianza kufanya kama wanafiki, wakiondoka katika ushirika na waumini wa mataifa wakati baathi ya wayahudi walikuja, aliwaingilia kwa sababu ***"njia yao haiendi sawasawa na ile kweli ya injili"*** **Wagalatia 2:14.** Mwanzo wa barua yake kwa wagalatia anasema ***"Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe"*** **Wagalatia 1:8.** Paulo alikuwa amemaanisha katika hii injili! Wewe umemaanisha? Imekuwa yako? Umeamua kuishi ama kufa kwa injili hii?

Paulo alimuandikia Timotheo, ***"Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu, wa uzao wa Daudi kama inenavyo injili yangu"*** **2 Timotheo 2:8.** Paulo aliamini katika injili – kwamba ni ***"uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye"*** **Warumi 1:16** na ni kwa sababu ya injili hii ambayo Paulo anasema anateseka na ***"Anastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule, ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele"*** **2Timotheo 2:10.**

Injili hii inatangaza kwamba kuna mfalme mpya na kwamba Amejipatia ushindi mukubwa! Yesu ndiye mfalme aliyeahidiwa, Kristo ambaye ameichukua enzi ya Daudi, ambaye anatawala kila kitu (**Isaya 9:7; Mt 28:18; Mdo 2:33),** Na ameshinda dhambi na shetani (**1 Yohana 3:5, 8; Wakolosai 2:15)** na ***"Aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile injili"*** **2:1-10**

**Anataka injili hii iimarike ndani yako ili iwe "injili yako!"**

### 2. Kulingana na "mahubiri ya Yesu Kristo"

Hakuna wengi leo ambao wanamhubiri Yesu kama Kristo. Wengi katika kanisa ulimwenguni kote wana ufahamu uliopunguka sana wa Yesu ni nani na inamaanisha nini kumuita **Kristo.** Maduka ya vitabu vya kikristo yamejaa mafundisho ya mikakati "yakuishi maisha yenye ushindi" na ujumbe wa kusisimua na hayana kitu kuhusu yaliyofunzwa na Yesu na Mitume.

Wakati Yesu aliuliza wanafunzi walidhani yeye kuwa ni nani Petro alitangaza, ***"Wewe ndiwe Kristo mwana wa Mungu aliye hai"*** **Mathayo 16:16.** Majibu ya Yesu yalikuwa, ***"…Na juu ya mwamba huu (ufunuo wa yeye ni nani), nitalijenga kanisa langu"*** **Mt 16:18.** Mara ya kwanza ambayo Yesu alitaja "kanisa" ilikuwa ni kwa ufunuo wa yeye ni nani!

**Twahitaji kufahamu na kuhubiri ufunuo ya kuwa Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu!** Paulo alisema kwa Tito ya kuwa tumaini la uzima wa milele na kutimizwa kwa ahadi za Mungu ***"Amelifunua neno lake kwa majira …kupitia mahubiri*** **(Tito 1:3).** Ni tunapo mhubiri Yesu aliye Kristo kwamba tunaimarishwa katika uhakika wa maisha yake. Neno linajidhihirisha (linakuwa hai katika ujuzi wetu) ikiwa tu imehubiriwa.

***"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake…"*** **Yohana 1:1, 14.** Mungu tena anataka Neno (ambaye ni Yesu Kristo) afanyike mwili, ajifunue katika mwili wa mwanadamu! **Neno linavyojidhihirisha kwa kuhubiri, ulimwengu utaona utukufu wake!** Tunapo lihubiri neno la Yesu aliye Kristo, tumaini la uzima wa milele linajidhihirisha na tunaimarishwa katika utukufu wake! Paulo alimwagiza Timotheo mbele ya Yesu Kristo ***"Alihubiri neno!"*** **2 Timotheo 4:2.**

### 3. Kulingana na "ufunuo wa siri"

Mungu anatuimarisha kulingana na ***"Ufunuo wa siri uliyositirika tangu ulimwengu ulipo anza, lakini sasa umefunuliwa".*** Tayari katika **Warumi 11:25** Paulo ataja kuhusu siri ya mataifa kuwa sehemu ya "***Shina na unono"*** **aya 17** ya ahadi zilizofanywa kwa waisraeli katika asiri. Siri ni kwamba Mungu ***"Atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia – katika Yeye"*** **Waefeso 1:10.** ***"Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu…Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu"*** **Wagalatia 3:26,28.**

Paulo anamuandikia Timotheo kuhusu ufunuo wa siri ya utauwa, ya kwamba ***"Mungu alidhihirishwa katika mwili"*** **1Timotheo 3:16.** Anasema siri hii haina shaka kuihusu; ni ***"Bila shaka".*** Ufunuo huu ndio unaofanya kanisa ***"nguzo na msingi wa kweli"*** **1 Timotheo 3:15.**
Mungu anavileta vitu vyote pamoja katika moja, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani – ndani yake! Mbingu na nchi zilikuja pamoja katika Yesu Kristo; Mungu alifanyika Mtu! Mungu

ambaye ni Roho **Yohana 4:24** akijidhihirisha katika mwili! Ufunuo huu wa kweli unapoimarishwa ndani Yetu, tunaweza kuona vyema yakuwa Mungu anatazamia kufanya jambo lilelile katika mwili wa Kristo. Anatujenga pamoja tuwe ***"Maskani ya Mungu katika Roho!"*** **Waefeso 2:22**

Mungu anawarejesha mitume na manabii tena kanisani siku hizi kuachilia ufunuo wa siri kwa watakatifu, hivyo kutuimarisha! **Waefeso 3:5**.

4. **Kwa "maandiko ya kinabii yakijulikana na mataifa yote"**

Yesu hajatuita tujenge makanisa makubwa na huduma ama kupata pesa kupitia biblia kama kitabu cha kujisaidia cha wasemaji wenye kusisimua. Yesu alituambia ***"Basi, enedeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza… na kuwafundisha…"*** **Mt 28:19-20.** Tunawafanya mataifa kuwa wanafunzi! Sio kufanya miondoko ya kanisa ama virabu visivyo wakaribisha wote. Tunawafanya mataifa kuwa wanafunzi kwa kuwajulisha kutimizwa kwa maandiko ya kinabii kwa watu wote!

Wakati Yesu alijitokeza kwa wanafunzi wake baada ya kufufuka katika wafu alisema, ***"Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambiwa nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika manabii na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko"*** **Luka 24:44-45.** Yesu alifanya yajulikane maandiko ya kinabii na kutimizwa ndani yake!

Paulo alisema kwamba kifo cha Kristo kwa dhambi zetu, kuzikwa kwake na kufufuka kwake siku ya tatu kulikuwa ***"kama yanenavyo maandiko"*** **1 Wakorintho 15:3-4.**

Siku ya pentekote ***"ilipotimia"*** **Mdo 2:1** Petro alisimama na kutangaza kutoka maandiko ya kinabii ya kuwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ilikuwa ni thibitisho kwamba huyu Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa **Mdo2:33.**

Wakati towashi wa Kushi alikuwa akisoma katika nabii Isaya, Filipo alimuuliza kama anafahamu. Mtu huyu wa Kushi alihitaji mtu wa kumsaidia na kwa hivyo Filipo ***"akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu"*** **Mdo 8:35.** Unaweza fanya maandiko ya kinabii yajulikane na mataifa yote?

Huduma ya kanisa ni kwa Mataifa! Ni kupitia neema na utume ambapo mataifa wanatii imani **Warumi 1:5**. Maandiko ya kinabii yaliandikwa wakati watu watakatifu wa Mungu walipelekwa na Roho Mtakatifu **2Petro 1-21**. Hayana utafsiri wa siri lakini yanatakiwa yafunuliwe kwa mataifa yote ili watu wote wapate kujua hakika kwamba Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa, Mungu katika mwili! **Mwanzo 49:10 Isaya 9:6**.

5. **Kulingana na "amri ya Mungu wa milele, kwa kuitii imani"**

Injili sio tikiti ya kwenda mbinguni. Injili ndiyo njia ambayo Mungu huleta mataifa katika kutii kwa neno lake! Paulo alisema kwamba kufunuliwa kwa neno la Mungu kupitia huduma ya kuhubiri ni kulingana na uwakili aliopewa ***"kwa amri ya mwokozi wetu mungu"*** **Tito 1:3.**

Tumaamrishwa kuhubiri injili na kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi (**Mariko 16:15, Mt 28:19**). Matokeo ya kutii amri hii ni ili mataifa watii imani na hivyo ufalme wa Mungu unaimarishwa. **Isaya** alitabiri siku hii katika **Isaya 2:2-4** akisema yakuwa mlima wa nyumba ya Bwana utaimarishwa juu ya milima – hivyo ni ***"juu sana kuliko ufalme wote na mamlaka na***

***nguvu na ushultani"*** **Efe 1:21** – na mataifa yote watafulika kwake. Watasema wanataka kufundishwa njia za ufalme wa Mungu na neno lake litahukumu na kukemea mataifa na matokeo yatakuwa, ***"Taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita kamwe"*** **Isaya 2:4.** Hallelujah!

Hii ni **kulingana na amri ya Mungu wa milele!** Itatendeka, haitazuilika, ***"Milango ya kuzimu haitalishinda kanisa"*** ambalo limejengwa na kuimarishwa katika ufunuo, likitii amri za Mungu!

Mataifa wakilitii neno la Mungu! Paulo alisema ***"Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu, Mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo"*** **Warumi 15:18.** Matunda ya injili ambayo tunatazamia ni ***kuitii imani.*** Mungu anatuimarisha kulingana na amri zake!

- **Ni wakati wa kuimarishwa katika injili hii**
- **Ni wakati wakuhubiri Yesu aliye Kristo**
- **Ni wakati wakuimarishwa katika ufunuo wa siri**
- **Ni wakati wakufanya Neno la kiunabii lijulikane na mataifa tote**
- **Ni wakati wa kuimarishwa kulingana na amri za Mungu kwa kuitii imani**

# TUMECHAGULIWA TUYAJUE MAPENZI YAKE

Wakati Paulo alikuwa akishuhudia mbele ya Wayahudi katika kitabu cha **Mdo 22**, aliyahesabu mambo ambayo mwanafunzi Anania aliyomwambia kwa neno la Bwana Yesu, ***"Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake, na kumwona Yule mwenye haki, na kusikia sauti itokayo katika kinywa chake. Kwa maana utakuwa shahidi wake kwa watu wote, wa mambo hayo uliyoyaona na kuyasikia"*** **aya 14-15.** Kuna mambo matano ya muhimu ambayo Anania alishiriki na Paulo ambayo twapaswa kuyafahamu na turuhusu mioyo yetu iyashike. Mwito wetu ni ule ule!

## 1) KUCHAGULIWA

Tumechaguliwa! Anania alitaka kwanza Paulo ajue kwamba alichaguliwa na Bwana! Mtu huyu ambaye ***"Akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana"*** **Mdo 9:*1*** alikuwa hakika ***"Chombo kiteule"*** cha Bwana Yesu **Mdo 9:15.**

### Kabla ya mwanzo wa nyakati

Hii ni siri ya neema ya Mungu ikifanya kazi katika maisha Yetu. Paulo anamwabia Timotheo ya kwamba Mungu ***"ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu si kwa kadri ya matendo Yetu sisi bali kwa kadri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo tangu milele"*** **2Timotheo 1:9.** Tumechaguliwa sio kwa sababu ya jambo nzuri ambayo tumeitenda lakini ni kwa kusudi la Mungu na neema yake! Paulo alisema kwamba alikuwa ***"Mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri"*** **1 Timotheo 1:13.** Mungu alikuwa na kusudi akimchagua Sauli na kuchagua kulitendeka katika Kristo kabla ya nyakati! Wakati tunaamua kuwa hakika na Yesu tunaingia katika mapenzi yaliotangulia kupangwa na mpango wa Mungu katika maisha Yetu.

Katika **Efe1:4** Paulo anaandika, ***"Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo".*** Kuchaguliwa kwetu ni katika Kristo na inatutenga kwake ili tuweze kutembea mbele zake. Petro anasema ***"Ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, Taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu"*** **1 Petro 2:9.** Kuchaguliwa kunakupa alama ya Yule aliye kuchagua! Unajua mahali pako na wewe ni wa nani!

### Kujua kuchaguliwa

Yesu alisema, ***"Si ninyi mlionichagua mimi bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa…"*** **Yohana 15:16.** Yesu anataka tujue ya kwamba yeye ndiye muanzilishi; yeye ndiye ***"Aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake"*** **1 Timothe 1:12.** Unapojua kwamba ni Yesu amekuchagua haijalishi kila ambacho mwanadamu anakufikilia. Wengi leo wanaokwamilia katika mipangilio ya kidini ambayo inaitwa "kanisa" hawana usalama katika nafasi zao kwa sababu ni nafasi zilizopeanwa – msingi wake hauko katika kuchaguliwa na kuitwa na Yesu.

Katika ujuzi wa Pulo alijua "kuchaguliwa bila shaka – Yesu alimfunza binafsi na pia kupitia Anania. Twahitaji kujua na kushawishika kwa kuchaguliwa kwetu na yeye. Kama

tumechaguliwa, hiyo inamaanisha sisi ni wake; sisi ni jukumu lake na tunaweza kuhakikishiwa kwamba tukiwa watiifu hatatuacha! Twahitaji kujua kwamba TUMECHAGULIWA!

## 2) KUYAJUA MAPENZI YAKE

Tumechaguliwa kuyajua mapenzi ya Mungu! Hatutakiwi kuyapuuza mapenzi yake. ***"Kwasababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana"*** **Efe 5:17**. Waamini wengi katika kanisa la sasa hawana ufahamu wowote wa mapenzi ya Mungu ni yapi. Tumejipatia katika kuokoa nafsi kama mpango wa kusudi la kipekee la Mungu ulimwenguni ni kuwapatia watu mahali mbinguni wakisha kufa.

### Kuyapatanisha mambo yote

Paulo anasema ya kwamba Mungu ***"Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake"*** **Efe 1:9.** Siri ya mapenzi ya Mungu ni kupitia ukombozi na msamaha ambao uko katika damu ya Yesu, Mungu sasa anaweza ***"kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vtote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia – katika yeye"*** **Efe 1:10.** Hallelijah! ***"Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake, kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni"*** **Wakolosai 1:19-20.**

Ni mapenzi ya Mungu kwamba vitu vyote vipatanishwe; vitu vyote vikiletwa katika moja! Hapana tena kutotii ulimwenguni, ***"Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari"*** **Isaya 11:9.** Ni makusudi ya Mungu kwamba dunia yote ipate kumjua yeye **(Yeremia 31:34)** na matokeo ya hayo yatakuwa ***"Mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake"*** **2 Petro 3:13.** Tunapoona nguvu za damu na sadaka ya Yesu ya kuvipatanisha vitu vyote, dhambi yetu inaondolewa na kuhukumiwa na haki inabaki. Wale ambao wanaendelea kutenda uasi na kuudhi, ***"kuwa ni adui za msalaba wa Kristo"*** **Wafilipi 3:18,** watakusanywa na kutupwa kwenye moto. ***"Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao"*** **Mt 13:43.** Tumepangiwa kuurithi ufalme wa Mungu duniani!

### Omba uyafahamu mapenzi yake

Paulo anasema kwamba ***"hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake"*** **1Wakolosai 1:9.** Maombi ya Paulo kwetu ilikuwa ili tuweze kuyafahamu mapenzi ya Mungu na tuweze kukua ndani yake ***"Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake…"*** **Efe 1:18**. Ni kwa kuwa na mawazo yetu yakifanywa upya na neno la Mungu ambapo tunaweza ***"Kujua mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza na ukamilifu"*** **Warumi 12:2.**

Ni mapenzi mema na ya kukubalika ya Mungu kwetu ***"tuishi maisha ya utulivu na amani katika utauwa wote na ustahivu"*** **1Tmotheo 2 :2-3.** Hii itatendeka wakati tunatii neno na kuwaombea watu wote na wale walio katika mamlaka. Ni mapenzi yake kwa ***"watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli"*** **1Timotheo 2:4.** Mungu anataka watu waokolewe kwa kujua ukweli! Tumechaguliwa **kuyajua mapenzi yake!**

Anania alimwambia Paulo alikuwa ayajue mapenzi ya Mungu na sehemu nzuri ya maandiko katika agano jipya ilikuja kutoka kwa mtu huyu. Alikuwa na ***ufunuo wa siri*** na sisi kama kanisa twatakiwa kutembea katika ufunuo huu. Hakika ni lengo la Mungu ***"Dunia ijazwe maarifa ya utukufu wa Bwana…"*** **(Habakuki 2:14).**

### Msikose kujua

Wandugu, haijakubaliwa tena sisi tuwe hatujui, ***"kwa maana ndugu zangu, sipendi msiijue siri hii, ili msijione kuwa wenye akili…"*** **Warumi 11:25.** Kama hatuna ufahamu wa mapenzi ya Mungu, ***"habari ya kusudi lote la Mungu"*** **Mdo 20:27,** italeta tu majivuno ya kidini katika kujua kwetu kuliko kulipokea neno kwa unyenyekevu kama ilivyo andikwa. Hatukuitwa kuzijenga dini zetu na vikundi vya mawazo yaliyogawanyika, lakini ni lazima tujengwe na tuje kwa ***"umoja wa imani"*** kwa maana tulichaguliwa **kuyajua mapenzi yake!**

### 3) KUMWONA YULE MWENYE HAKI

Ulijua umeitwa umwone Yesu! Anataka umwone! Anatamani umwone kama alivyo. ***"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo"*** **1 Yohana 3:2.** Twayatupilia maandiko haya hata nyakati za mwisho. Lakini haijasema ya kuwa haya hayawezi kukamilika lakini ***"atakapodhihirishwa …tutamwona kama alivyo".*** Yesu amejidhihirisha kwako? Umemwona?

### Kumwona - ufunguo wa urithi.

Katika **2 Wafalme 2** tuna hadithi ya Eliya akichukuliwa na upepo wa kisulisuli. Elisha alikuwa mtumishi wa Eliya, ***"Aliyekuwa akimimina maji juu ya mikono yake Eliya"*** **2Wafalme 3:11.** Eliya alipokuwa akifanya safari yake ya mwisho katika vikundi vyote vya manabii aliendelea kumuuliza Elisha abaki nyuma na awaangalie manabii katika mji huo. Mara walipo vuka Yorodani kimiujiza Eliya akamwambia Elisha ***"Omba kwangu lolote utakalo nikutendee kabla sijaondolewa kwako"*** jawabu ya Elisha ilikuwa ya ajabu, "***nakuomba sehemu maradufu ya roho yako na iwe juu Yangu"*** **2Wafalme 2:9.** Eliya alisema**, "*Umeomba neno gumu; lakini, ukiniona nitakapoodolewa kwako utalipata, la hukuniona hulipati"*** **Aya 10.** Elisha alitaka **sehemu maradufu.** Hii ni haki ya wana wazaliwa wa kwanza. Eliya alitaka urithi, sio kubaki akiwa mtumishi, lakini awekwe katika uwana. Ilitegemea yeye **kuona!**

Kisha ikatendeka ya kuwa Eliya alichukuliwa mbiguni na upepo wa kusulisuli na tazama kukatokea **gari la moto na farasi wa moto (2 Wafalme 2:11).** Elisha **"akaona, akalia, Baba yangu, baba yangu, gari la Israeli na wapanda farasi wake!" Aya 12.** Ni gari gani ambayo Eliya aliona? Ni kitu gani kilikuja kwake ambacho kilimbadilisha mara **kutoka kwa uhusiano wa mtumishi na Bwana mpaka kwa kulia "Baba yangu baba yangu"?**

### Gari

Ezekieli anasema katika mwanzo wa kitabu chake cha kinabii kuwa, ***"Mbingu zilifunuka, nikaona maono ya Mungu"*** **Ezekieli 1:1.** Kisha anasema ***"Na tazama upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini, wingu kubwa sana, pamoja na moto, ukifanya duara ya nuru, na mwangaza pande zote...,"*** **aya 4.** Pahali hapa pa kushangaza palikuwa pangumu kuelezea lakini alisema viumbe vinne vyenye uhai zilikuja ndani yake, sura yake ikiwa kama ***"makaa ya moto yawakayo"*** **aya 13,** na palikuwa na gurudumu kando ya kila kiumbe na ikageuka kila pande iliyotaka kwenda! ***"Na juu ya anga, lililokuwa juu ya vichwa vyao, palikuwa na mfano wa kiti cha enzi…na juu ya mfano huo wa kiti cha enzi, ulikuwako mfano kama kuonekana kwa mfano wa mwanadamu juu yake"*** **aya 26.**

Hallelujah! Gari la Israeli ni kiti enzi ya Mungu na mmoja kwa mfano wa mwanadamu anaketi katika juu ya enzi hii. Elisha aliona nini? Aliona kiti enzi! Alimwona Yule aketiye katika "gari la Israeli"! Eliya katika maisha yake **alisimama mbele ya Yahweh** na angeamuru viumbe

yatakavyofanya (**1 Wafalme 17:1).** Elisha alitaka sehemu maradufu, urithi wa roho ya Eliya. Alichokiona wakati Eliya alichukuliwa ilikuwa sio kitu spesheli kuhusu Eliya, lakini alimwona Yule ambaye Eliya alisimama mbele yake na wakati huo akafanyika kuwa mwana, sasa akiweza kutembea katika urithi! Alimwona Mungu; aliona kiti enzi! Mungu alifanyika Baba yake! Sasa Eliya akawa na msimamo kama Eliya **(2 Wafalme 3:14**)! Tumechaguliwa kuona **Yule mwenye haki!**

## Ayubu aliona na kupokea urithi!

Ayubu alikuwa mtumishi mzuri wa Mungu, akiyafanya mambo yote vyema, akifanya sadaka zilizofaa, akiwasaidia maskini, wajane, mayatima na kuwa mzee katika mji. Alikuwa na jamii kubwa na kuwa na mifugo wengi na alikuwa akitenda vyema hadi wakati wa majaribu ulipofika. Mungu alitaka kuboresha uhusiano wake na Ayubu – Alitaka kumleta katika urithi wake wa kiroho!

Wakati ulipofika, ***"ndipo Yahwe akamjibu Ayubu katika upepo wa kisulisuli"*** **Ayubu 38:1.** Baada ya Mungu kuzungumza na yeye juu ya yale yote aliyoyatenda katika kuumba, akizitangaza nguvu zake, Ayubu alisema kwake ***"Nilikuwa nimesikia habari zako, kwa kusikia kwa masikio; bali sasa jicho langu limekuona"*** **Ayubu 42:5.** Mungu alitaka kujifunua kwa Ayubu. Sasa Ayubu alitambua kwamba alichaguliwa ili ***KUMUONA*** Yule mwenye haki. Kisha, ***"Yahweh akaugeuza uteka wa Ayubu, hapo alipowaombea rafiki zake; Yahweh naye akampa Ayubu mara mbili kuliko hayo aliyokuwa nayo kwanza"*** **Ayubu 42:10.** Baada ya Ayubu kumwona Yahweh, alipokea sehemu maradufu, urithi wa mwana!

## Yesu aliona na kuupokea urithi!

Wakati Yesu alitimiza umri ulikuwa ni wakati wake kwenda kukutana na Yohana mbatizaji katika Yordani kwenda kubatizwa. ***"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake"*** **Mathayo 3:16.** Katika injili ya Luka anasema Roho alishuka ***"Kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua"*** **Luka 3:22.** Yesu ALIONA na akapokea Roho. Mara tu baada ya haya, sauti ilikuja kudhibitisha na kumweka katika mahali pa mwana aliyekomaa – akiweza kutembea katika urithi! **Mathayo 3:17**.

Tumechaguliwa kuwa na mbingu zilizotufungukia, kumwona Yule mwenye haki. Ni hatima yetu kusimama mbele ya enzi yake na kumwona katika utukufu wake. Wakati Yesu alipomchukua Petro, Yakobo na Yohana juu ya mlima ***"Akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru"*** **Mathayo 17:2.** Petro anasema katika waraka wake kwamba ***"…hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake"*** **2 Petro 1:16.** Walimwona kama vile alivyo, walikuona kuja kwake! Walimwona mwenye haki!

***"Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hadi utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho"*** **2 Wakorintho 3:18.**

Anania alimwambia Paulo kwamba alichaguliwa amwone Yule mwenye haki. Yesu anataka wewe umwone! Itakubadirisha – itakuwezesha kutembea katika urithi wako, itakuwezesha kuwa kama yeye!

## 4) KUSIKIA SAUTI YA KINYWA CHAKE

Hatujachaguliwa tu kumwona Yesu lakini tumechaguliwa tusikie sauti ya kinywa chake! Hallelujah! Mungu anataka umusikie. Kutembea kwa imani yamaanisha twatakiwa tumsikie kwa sababu ***"Imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"*** **Warumi 10:17.** Hapo mwanzo baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi inasema ***"Kisha wakasikia sauti ya Yahwe Mungu, akitembea bustanini…"*** (**Mwanzo 3:8**). Adamu na Hawa hakika **walisikia sauti ya Yahweh akitembea!** Umemsikia wewe! Mungu ni waajabu na anataka tujue na tujifahamishe kusikia sauti Yake!

### Kondoo wangu husikia sauti yangu

Katika **Yohana 10** Yesu anafundisha kuhusu yeye akiwa mchungaji mwema na kwamba wale wote wanaokuja katika zizi lake lazima waje kwa njia iliofaa. Katika **aya 4** Yesu anasema, ***"Naye awatoapo nje kondoo wake wote, huwatangulia; na wale kondoo humfuata kwa maana waijua sauti yake".*** Kondoo wa Mungu hujua sauti yake na humfuata – wanafuata sauti inayo watangulia.

### Maisha ya kufufuka inaachiliwa kwa kusikia sauti yake

Ni kwa kusikia sauti ya Mwana wa Mungu tunavuka kutoka kifo mauti kwa uzima! ***"…yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. …saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya mwana wa Mungu, na wale waisikiayo watakuwa hai"*** **Yohana 5:24-25.** Sauti ya Mungu ina nguvu sana kwamba inaweza hata kufufua wafu! Umezaliwa mara ya pili jinsi gani? Kwa kulisikia neno la Mungu ambalo lilihuisha moyo wako, **"*…mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isioharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele"*** (**1 Petro 1:23**).

Hata Lazaro alipokuwa amekufa kwa siku nne, Yesu akimwombea na akiugua katika Roho, ***"Akalia kwa sauti kuu, Lazaro joo huku nnje! Akatoka nje Yule aliyekufa…"*** **Yohana 11:43- 44.** Hii ilikuwa ishara ya siku ***"ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu"*** **Yohana 5:28:29** sauti ya Mungu hakika ina nguvu na ***ina adhama*** **(Zaburi 29:4)**

### Uasi unaangamizwa na sauti ya kinywa chake

Paulo anasema kwa barua yake kwa Wathesalonike kwamba, ***"hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumuangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake"*** **2 Wathesalonike 2:8**. Ni kwa Neno Lake, sauti ya kinywa chake, na kwa kumwona, nuru ya kuja kwake ambapo yule asi ataangamizwa! Watu wengi wanafahamu hii inanena kuhusu nani lakini katika maisha yetu twaweza kuyaona haya yakifanya kazi.

Sauli alikuwa mtu muasi. Hata kama alikuwa ni mmoja wa watu wakuu walioilinda sheria alijipata akipigana na Mungu kwa kulitesa kanisa. Wakati Yesu alimjia na akanena, yule asi ndani yake alifunuliwa na akaangamizwa! Tunapomwona Yesu na kusikia sauti ya kinywa chake, yule asi ndani mwetu anafunuliwa na kuangamizwa!

Katika **Isaya 11:4** nabii anasema kwamba yesu ***"Ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake, na kwa pumzi ya midomo yake atawauwa wabaya".*** Ni kwa sauti ya Mungu ikinena kupitia Mwana (**Ebr 1:2**) kwamba maovu yote itaangamizwa na kuchomwa na ni haki tu

itakayobaki! ***"Je, neno langu si kama moto? Asema Yahweh"*** **Yeremia 23:29.** Wakati moto wa neno la Mungu linapita kunabaki tu ***"mbingu mpya na nchi mpya ambayo, haki yakaa ndani yake"*** **2 Petro 3:13**

### Sauti yake nikama maji mengi

Yohana anasema katika **Ufu 1:15** ya kwamba, ***"Na sauti yake kama sauti ya maji mengi".*** Ezekieli aliijua sauti iyo hiyo, ***"…kama mshindo wa maji makuu, kama sauti yake mwenyezi, mshindo wa mvumo, kama mshindo wa jeshi…"*** **Eze 1:24.** Sauti ya Yesu ni kama sauti ya mshindo wa mvumo, kama mshindo wa Jeshi! Yesu ni Mungu aliye miongoni mwa watu wake ambao wamejitayarisha kwa sababu ya vita.

Mtume Paulo anasema kwambaYesu analipenda kanisa na alijitoa kwa sababu yake ili, ***"Alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi…"*** **Waefeso 5:26-27.** Kwa neno anatuosha kama kwa maji na inatufanya kuwa kanisa lenye utukufu, lililokomaa la wale walioitwa – jeshi linaloonyesha utukufu wa Yesu mwenyewe. Ni kwa sauti yake, neno lake. Neno la Kiyunani lililotumika la "Neno" katika aya hii ni "Rhema" ambayo ni neno lililohuishwa, lililonenwa ambalo limetoka katika kinywa chaMungu – ni kwa "kusikia sauti ya kinywa chake" ambapo tunatakaswa na kuoshwa tuwe kamili! Maji ya neno lake inatutakasa, ***"ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililo waambia"*** **Yohana 15:3**

**Tumechaguliwa kusikia sauti ya kinywa chake!**

### 5) UTAKUWA SHAHIDI WAKE KWA WATU WOTE

Unapochaguliwa kuyajua mapenzi ya Mungu, kumwona, na kumsikia kisha unapewa uweza wa kumshuhudia kwa watu wote! Tunaweza kuwa tu mashahidi wa yale ***"tumeyaona na kuyasikia"*** **(Mdo 22:15)**

### Neno ni mtu wa kujuana naye

Mtume Yohana anaaza barua yake kwa kusema, ***"Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya neno la uzima – (na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, nasi twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu)"*** **(1 Yohana1:1-2).** Mitume wa kwanza walipata kujionea uhakika wa ***"Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake…"*** **(Yohana 1: 14),** na kwa sababu ya haya waliweza kushuhudia kwa watu wote wakiwaleta watu katika ***"Ushirika na Baba na mwana wake Yesu Kristo"*** **(1 Yohana 1:3).**

Yesu anatakiwa kujulikana! Tunaweza tu kushuhudia kwa watu mambo tuliyoyaona ama kusikia ama kugusa ama kuoja! ***"Onjeni mwone ya kuwa Yahweh yu mwema*** **(Zaburi 34:8).** Unao ushuhuda wa kibinafsi wa Yesu? Mtume Paulo alikuwa na uweza wa kutumia ushuhuda katika hali mbili kwa mkutano wa hadhara kama iliyo nakiliwa katika kitabu cha **mdo**. Paulo akawa shahidi!

### Twahitaji Roho Mtakatifu ili tushuhudie

Uhakika wa kumjua Yesu huja kupitia Roho Mtakatifu na ni kwa Roho Mtakatifu wa Mungu ambapo tunapokea nguvu za kushuhudia. Mtume Paulo anaandika, ***"…hakuna awezaye kusema Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu"*** **1 Wakorintho 12:3.** Tunampata

Yesu kwa Roho wa Mungu, kwake ***"macho ya ufahamu wetu yakitiwa nuru"*** **(Efe 1:18).** Yesu aliwaambia mitume kwamba ***"… mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu…"*** **(Mdo 1:8).** Tunamhitaji Roho wa Mungu ***"Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho wa unabii"*** **Ufu 19:10.**

Yesu alisema, ***"Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia. Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami"*** **(Yohana 15: 26-27).** Tunahitaji mambo mawili ili tuwe mashahidi – tunahitaji kumpokea Roho ambaye hushuhudia kumhusu Yesu na tunatakiwa tuwe na Yesu, tukiwa tumejifunza kutoka kwake, kusikia kutoka kwake, na kumpapasa.

### Ni wakati wa kuwa halisi na Yesu!

Haijatosha kuwa na mambo fulani ya kihistoria kumhusu Yesu na aliyoyatenda. Hajatosha pia kuwa na ufahamu wa maandiko. Paulo alikuwa mfarisai wa wafarisai; alijua Biblia, alikuwa na juhudi za aliyemdhani Mungu kuwa. ***"Nami niliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabila yangu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu"*** **(Wagalatia 1:14).** Lakini alipokutana na Bwana Yesu aliyefufuka alilia, ***"U nani wewe, Bwana?"*** **(Mdo 9:5).** Kupitia kujifundisha kwake kote na kujifundisha katika sheria, hakumjua Bwana! Wakati alikutana na ufunuo wa Mungu katika uhakika, akatambua hakuwa amemjua Bwana; mara tu akauliza, ***'U nani wewe Bwana?'*** hakumjua BWANA!

***Mungu anawatafuta watu watakaokuwa na ujasiri kusimama na kushuhudia Yesu katika maisha yao kulingana na neno la Mungu.***

***Anataka tumjue Yeye ili tupatiane ushuhuda wa kweli wa kile tumeona na kusikia.***

***Mtafute Mungu, mjue na ushuhudie kwamba huyu Yesu ndiye Kristo/Masihi, Mwana wa Mungu, Mungu aliyethihirishwa katika mwili!***

# KUDHIHIRISHWA KWA JINA

### Nimelidhihirisha jina lako

Wakati Yesu alikuwa akimwomba Baba usiku kabla ya kusulubiwa kwake, alikuwa akitoa hesabu kwake jinsi alivyokuwa ***"amemaliza kazi"*** ambayo alikuwa amepatiwa (**Yohana 17:4).** Katika **aya 6** Yesu anasema mojawapo ya kazi kuu ambayo alikuwa amekamilisha ni "***Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu".*** **Yesu alidhihirisha jina la Baba!** Hii ni ya ajabu sana na ndani yake kuna ufunuo kwetu katika kueleza Yesu ni nani.

Katika **1 Wakorintho 3:11** Paulo anaandika, ***"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo".*** Ule ***"msingi imara"*** ambao tunaweza kujenga juu yake ni katika ufunuo wa kujua Yesu aliye Masihi ni nani. Katika wakati ambapo Yesu alikuwa awaache wanafunzi na kwenda msalabani na kufufuka tena Alimwambia Baba kwamba nimefaulu ***"kudhihirisha jina Lako". Yesu alikuwa akisema yeye ndiye uthihirisho wa jina la Baba!*** Ambaye Yesu ndiye inafunua Baba***! "Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili"*** **Wakolosai 2:9**

Katika **1Timotheo 3:16** Paulo anaandika siri ya utauwa ni kuwa ***"Mungu alidhihirishwa katika mwili".*** Katika sura hii, tunataka kutazama jinsi Yesu angesema ***"Nilidhihirisha jina lako".***

- Yesu alidhihirisha jina la Mungu jinsi gani?
- Ni kwanini Yesu ni jina juu ya majina yote?

Twaona Filipo katika Samaria ***"Akazihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina la Yesu Kristo"*** **Mdo 8:12. Filipo alilihubiri jina!** Kuna ufunuo wetu wa kupokea ambao ni wa kimsingi katika imani Yetu. Ufunuo uko katika jina la Mungu!

### Jina la Mungu likifunuliwa katika agano la kale

Mungu alijifunua mara nyingi katika agano la kale kwa jina lake. Lakini katika tukio moja spesheli alijitabulisha wazi kwa musa akisema, ***"Hili ndilo jina langu hata milele, nalo ni kumbukumbu langu hata vizazi vyote"*** **Kutoka 3:15.** Mungu alitaka kumtuma Musa kuwakomboa watu wake toka nchi ya Misri na kutoka kwa utawala wa Farao, na Musa akamuuliza Mungu, ***"Nitakapofika kwa wana wa Israeli, na kuwaambia, Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wakaniuliza, jina lake n'nani? niwaambie nini?"*** Mungu alijibu kwa kusema ***"MIMI NIKO AMBAYE NIKO; akasema, Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli; MIMI NIKO amenituma kwenu"*** (**Kutoka 3:13-14).** Jina ambalo Mungu alilidhihirisha kwa Musa ambalo litakuwa ***"kumbukumbu hata milele kwa vizazi vyote"***, lilikuwa jina la milele **"MIMI NIKO".**

Katika Kiebrania ni jina **Yahweh** ama **Yehova** ama **Jehovah**. Inamaanisha ya kwamba **yeye ndiye wa milele; ambaye amekuwako siku zote, yuko kila wakati na atakuweko ziku zote.**

Jina lake linadhihirisha alivyo. Kuwa na ufunuo wa jina la Mungu ni kuwa na ufunuo wa yeye ni nani. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alisema kwamba hatua ya kwanza ya imani ni kuamini ya kwamba ***"Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamfafutao"*** **Wabrania 11:6.**

Katita tafsiri ya biblia katika kingereza, nyingi zimetafsiri jina kuwa **"BWANA"**. Hii sio tafsiri nzuri ya jina kwa maana jina lake halijamaanisha "Bwana". Tutatazama baadaye ni kwa nini hii ilitafsiriwa hivyo na jinsi Yesu ni udhihirisho wa kichwa!
Yesu alisema kwamba **alilidhihirisha jina la Baba**. Yesu ndiye udhihirisho wa jina la Mungu katika mwili (**1Timotheo 3:16, Yohana 1:1,14).**

## YESU ALIDHIHIRISHA JINA KWA NJIA GANI?

### Jina la Yehova (La Yahweh) majina ya Mungu

Kuna mara tisa katika agano la kale ambapo Mungu anatumia jina lake **"Yehova"** kama jina linalofunua kitu cha asiri yake ya milele. Tutatazama kila moja na tuone jinsi Yesu amedhihirisha jina lake katika maisha yake, akidhihirisha yeye ni nani.

### 1) YEHOVA YIRE – "MIMI NIKO nitapatiana"

Katika **Mwanzo 22**, Ibrahimu alikuwa akipokea mtihani mkuu sana kutoka kwa Mungu. Mungu alisema, ***"Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia"*** **(aya 2).** Hii ilikuwa ikionyesha jinsi Mungu atakapo mtoa ***"Mwana wake wa pekee"*** **(Yohana 3:16).** Mwana wa Ibrahimu alikuwa afanyike sadaka. Mwana aliyepatianwa kama ahadi kwa Ibrahimu alikuwa atolewe kama sadaka ya kumpendeza Mungu.

Katika **Aya 7,** Isaaka anashangaa ni nini kinatendeka na akamuuliza Ibrahimu, ***"Babaangu!... Tazama! moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa"***, Isaaka alijua kwamba Mungu alihitaji kondoo kwa sababu ya sadaka ya kuteketeza! Ibrahimu akajibu, ***"Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanagu"*** **(aya 8).** Kisha Ibrahimu akaendelea kumfunga Isaaka kwa madhabahu na alikuwa karibu kumchija mwanawe wakati Malaika wa Yehova alimuita akisema wacha. Wakati Ibrahimu alitazama aliona mwana kondoo akiwa ameshikwa kwenye kichaka na akamchukua mwana-kondoo na akamtoa sadakaya kuteketeza (**aya 12-13**).

Ibrahimu kisha akawa na ufunuo wa jina la Mungu kuwa ***"Yehova- yire, kama watu wasemavyo, hata leo, katika mlima wa BWANA itapatikana"*** **(aya 14).**

### Ninani atupatiaye?

**Yesu ni kipawa cha Mungu kwetu!** Katika mlima wa Bwana imepatianwa! Baada ya Yesu kubatizwa, ***"Yohana amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana -kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu, kwa maana alikuwa kabla yangu"*** **(Yohana 1:29-30).** Jua ya kwamba zawadi ya Mungu ***ni Mwana-kondoo.*** Mwana-kondoo huyu ni sadaka wa kuzichukua dhambi za ulimwengu. Hata kama Yesu alizaliwa baada ya Yohana, Yohana anasema mtu huyu, ambaye ni Mwana- Kondoo wa Mungu, ***"alikuwa mbele yangu".*** **Yesu ndiye wa milele ambaye ni zawadi ambayo Mungu amefanya kwa sababu ya dhambi za ulimwengu!**

***"Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhammbi…"*** **(1Yohana 3:5).** Katika **Ufunuo 13:8** tunaona ya kwamba zawadi ya Mungu ilikuwa ya milele, ***"Mwana- kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa kwa misingi ya dunia".*** Kutoka msingi wa ulimwengu kipawa hiki kilikuweko. Mungu wa milele, Yehova, ndiye alidhihirishwa kuzichukua dhambi zetu, kuwa zawadi yetu.

***Yesu amedhihirisha jina, "Yehova Yireh".***

**2) YEHOVA ROPHEKA – "MIMI NIKO mponyaji wako"**

Katika **kutoka 15:26** Mungu wa milele anajidhihirisha kuwa Yule ***"atuponyaye".*** Tunaponywa na jina la Yule atuponyaye. Wakati wana wa Isreli walitoka Misri, ambayo inazungumza juu ya watu wa Mungu wakitoka ulimwenguni na kuingia katika ufalme wa Mwana wa Mungu (**Wakolosai1:13**), walifika mahali penye maji machungu. Watu walinugunika na Mungu akamwonyesha Musa jinsi la kufanya na maji yakawa matamu. Mungu akafanya amri akasema, ***"Kwamba, utaisikiza kwa bidii sauti ya BWANA, Mungu wako, na kufanya yaliyoelekea mbele zake, na kuyatega masikio uyasikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia ndani yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisiri; kwa kuwa mimi ndimi BWANA nikuponyaye".*** Ahadi ya Mungu kwetu ni kwamba yeye ndiye mponyaji wetu na hapana mogonjwa yote ya dunia yatakuwa nasi.

**Ni nani mpoyaji wetu?**

**Mathayo** aliandika mapema katika huduma ya Yesu, ***"Na habari zake zikaenea katika Shamu yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza; akawaponya"*** **(Mathayo 4:24).** Katika **Mathayo 9:35** tunamwona Yesu tena, ***"Akiponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina".*** **Yesu ndiye atuponyaye!**

Wakati mitume waliachiliwa na Roho Mtakatifu baada ya Yesu kufufuka katika wafu, waliondoka wakihubiri. Katika **Mdo 3** tunamwona Petro na Yohana wakikutana na kiwete aliyekuwa akiomba nje ya hekalu. Katika **aya 6** Petro akasema, ***"Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa Jina la Yesu wa Nazareti, simama uende".*** Petro alitumia jina la Yule atuponyaye na kwa mamlaka yake yule kiwete akainuka!

Wakati Petro alikuwa akieleza sababu za uponyaji wa mtu huyu aliwaambia watu, ***"Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia mtu huyu nguvu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote"*** **(Mdo 3:16).** Petro hakuwa na shaka na jina! Katika **Mdo 4:10** ilibidi petro kuzungumza na watawala wa watu kuhusu uponyaji huo wa ajabu na akasema, ***"Jueni ninyi nyote na watu wa Isaraeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu"***

Jina ambalo Mungu ametupa ambalo linaleta uponyaji kwa watu ni **jina la Yesu! Yeye ndiye mponyaji wetu!**

***Yesu amedhihirisha jina la "Yehova Ropheka"!***

**3) YEHOVA NISSI – "MIMI NIKO Bendera yako"**

Sio kitambo sana baada ya wana wa Israeli walikuwa wameondoka toka mahali pa uponyaji wakakutana na adui. Wameleki wakawainukia na wakawa katika vita wakati Musa alikuwa katika mlima akiongoza vita akiwa na ***"Ile fimbo ya Mungu nitakuwa nayo mkononi mwangu. Ikawa, Musa alipouinua mkono wake, Israeli walishinda; na alipoushusha mkono wake, Ameleki walishinda"*** **(Kutoka 17:9, 11*).*** Ilimpasa Musa kushikilia fimbo ya mamlaka ya Mungu, na wakati fimbi ilishikiliwa walipokea ushindi! Watu wawili walipaswa kumsaidia ili aiweke mikono yake juu na wakashinda vita (**aya 12-13**).

Kisha ***"Musa akajenga madhabahu, akaiita jina lake YEHOVA nisi"*** **(Kutoka 17:15).** Yule wa milele alijidhihirisha kama bendera yetu, ambaye hutupa ushindi. Tunapigana chini ya jina lake. Maelezo katika Spirit Filllled Life Bible yasema kwamba "*Bendera ni kama kikingi*

*ambacho watu walitegemea. Wakati kiliinuliwa, iliwakusanya watu kwa vita, kwa mikutano au maagizo. Msemo ule ungekuwa ni kilio cha vita!*

Mungu wa milele ndiye bendera yetu. Tunakuja chini yake na kupata mahali pa kujificha. Wakati **fimbo ya mamlaka** yake imeinuliwa tunaingia na kupokea ushindi. Tunapolilia Jina lake liwe bendera yetu tunapata ushindi dhidi ya maadui zetu!

### Bendera yetu ni nani?

Wakati Yesu alijua kwamba anakaribia wakati wa kufa alisema, ***"Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu. Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayo kufa"*** **(Yohana 12:31-33).** Wakati wa kuhukumu adui wa Mungu ulikuwa umetimia, na Mungu angelifanya hayo kwa njia ya **Yesu kuinuliwa duniani! Yesu ni Bendera yetu ya ushindi"!**

Yesu alitwaa ushindi kwa ***"Kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutustaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani; akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo"*** **(Wakolosai 2:14-15).** Dhambi na shetani walishindwa na Yesu, fimbo ya Mungu ya mamlaka ikiwa **imeinuliwa hapa ulimwenguni! "*Kwa kusudi hili mwana wa Mungu alidhihirishwa ili azivunje kazi za ibilisi"*** **(1Yohana 3:8).**

***Yesu amelidhihirisha Jina la "Yehova- nisi"!***

### 4) YEHOVA M'KADDESH – "MIMI NIKO Utakaso wako"

Yule Mungu wa milele ndiye unayetutakasa na kuwatenga watu wake kwa ajili yake na kwa mambo yote yaliyo chukizo kwake. Katika kitabu cha **Walawi** Yahweh anapatiana maagizo yake na sheria jinsi inawapasa watu kukaa na maadiri mema, kutakasa na kuabudu na kumwendea yeye katika hali ya ukuhani, sadaka na Hema zikiwekwa. Katika **Walawi 20,** Yahweh anawaambia Waisraeli ya kuwa mtu awaye yote akigeuka kutoka kumwabudu Mungu wa kweli na amuabudu Molech au azigeukie pepo na wachawi kwa kuelekezwa **"*Nitamtenga na watu wake"*** **(aya 6).** Kisha akawaambia Waisraeli ***"Jitakaseni basi, iweni watakatifu kwa kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu, Nanyi zishikeni sheria zangu na kuzitenda; Mimi ndimi BWANA niwatakasaye ninyi"*** **(aya 7-8)**. Ni kwa kuyafuata maagizo yake na kuyatenda mapezi yake ambapo anatutenga kwa ajili yake.

### Ni nani utakaso wetu?

Mtume Paulo anaandika kwamba **"*Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi"*** **(1 Wakorintho 1:30).** Mungu sasa anatutakasa kupitia Yesu Kristo - Yeye ndiye utakaso wetu kutoka kwa Mungu! Tumetengwa na yeye na kwa ajili yake. ***"Maana yeye atakasaye na wale wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; akisema, Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu"*** **(Waebrania 2:11-12).** Yesu ndiye Yule anayetutakasa na hivyo hahaibiki kulitangaza jina la Mungu miongoni mwa ndugu zake. Yesu alisema, "***Jina lako nimewedhihirishia watu wale ulionipa …"*** **(Yohana 17:6).** Ni kwa jina lake ambapo tunatengwa!

### Kutakaswa kwa jina

Baada ya kuwaeleza Wakorintho jinsi hatuwezi kuurithi ufalme kama tunahusika katika utendaji dhambi na uasherati na kutaja aina ya dhambi ambazo zilikuwa zimekidhiri katika watu

wao (kama ilivyo kwetu pia), anasema, ***"Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu"*** **(1Wakorintho 6:11).** Hakika tunatakaswa katika **Jina la Bwana Yesu!**

Haya hutemdeka kwa jinsi gani tukieleza?

- Kwanza ni kwa kuliitia jina la Yesu kwa sababu ya wokovu wetu (**Warumi 10:13***)*
- Kisha kwa kubatizwa katika hilo **Jina – "*lakini mlioshwa"***
- Jina la **Yesu** linatutenga kwa Mungu kwa sababu ya huduma yake
- Jina la **Yesu** linatutakasa na kutuosha kama kwa njia ya ubatizo. Tunabatizwa ndani ya ***"Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu"*** **(Mathayo 28:19).**
- Neno ambalo linadhihirisha uungu wote-utimilifu wa Mungu – ni jina la **Yesu**. Anania alimwambia Paulo "***Simama, ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake"*** **(Mdo 22:16).** Petro aliwaambia wandugu ambao mioyo yao ilikatwa kwa kuhubiri kwake kwamba iliwapasa, ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo , mpate ondoleo la dhambi"*** **(Mdo 2:38).**

***Yesu alilidhihirisha jina la "Yehova M'Kaddesh"!***

### 5) YEHOVA SHALOM - "MIMI NIKO Amani Yako"

Katika kitabu cha **waamuz**i kuna hadithi ya mtu aliyeitwa Gidioni ambaye aliishi nyakati ambapo Waisraeli walikuwa wamegandamizwa na maadui zao, Wamidiani. Gidioni alikuwa akipuliza ngano! Kati ya siku zake, Yahweh, Yule wa milele, akamtokea kama **Malaika wa Yahweh (Waamuzi 6:12).** Ni wakati baadaye tu ambapo Gidioni alitoa sadaka kwa Yahweh ambapo alitambua aliyemuona na akalia, ***"Ole wangu, Ee Bwana MUNGU! Kwa kuwa nimemwona Bwana uso kwa uso. BWANA akamwambia, Amani iwe pamoja nawe; usiogope; hutakufa. Ndipo Gideoni akamjengea BWANA madhabahu hapo, akaiita jina lake, Yehova - Shalomu, {BWANA ndiye amani}"*** **(Waamuzi 6:22-24).**

Ni kupitia sadaka ambapo malaika wa Yahweh alijidhihirisha kwa Gideoni. Katika hadithi hii unaona kwamba **Malaika wa Yahweh** ni sawa na **Yahweh.** Yanatumika yote ukisema **Malaika wa Yahweh** anaongea na kusema **Yahweh** anaongea. Gideoni alimwona Yahweh katika Malaika wa Yahweh! **Tunamwona Mungu katika Yule Mungu amemtuma!** Yesu alisema ***"Aliyeniona mimi amemwona Baba"*** **Yohana 14:9,** naye ***"Anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma"*** **(Mathayo 10:40).** Gideoni alimwona Yahweh na kwanza akaogopa maana Mungu alikuwa amemwambia Musa ***"Huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi"*** **Kutoka 33:20.** Lakini Paulo anaandika kwamba, ***"Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo"*** **2 Wakorintho 4:6. Gideoni aliona YESU! Na Alidhihirishwa kupitia sadaka kama amani yake!**

### Amani yetu ni nani?

***"Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Kwa maana yeye diye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga… Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu. Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja"*** **(Efe 2:13-14, 17-18).** Amani

imekuja kwa damu ya Yesu Kristo. Amani na Mungu na amani na mmoja na mwengine. **Yesu ndiye udhihirisho wa amani ya Mungu! YEYE NDIYE AMANI YETU!**

**"*Kwa kuwa katika Yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni*" Wakolosai 1:19-20.** Hakuna tena utengano kati ya Mungu na wanadamu, kati ya mbingu na nchi, kwa sababu uungu wote unakaa ndani ya Yesu na kwa yeye ameleta vitu vyote pamoja na kufanya **AMANI!**

### Yesu alihudumu amani

Kabla ya msalaba Yesu alikuwa akizungumza na wanafunzi wake kuhusu kuondoka kwake na akasema, ***"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa, niwapavyo mimi sio kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga"* Yohana 14:27.** Aliongea vivyo hivyo kwa Gideoni! Aliwahudumia ndugu zake amani alipowaambia msiogope! Alikuwa karibu kumwangamiza yule aliyewashika watu wote mateka kwa hofu ya mauti (**Waebrania 2:14-15).** Kisha akasema kwao, ***"Hayo ninawaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu"* Yohana 16:33.** Tuna amani ndani ya **YESU!**

Baada ya kufufuka yesu aliwatokea wanafunzi wake ndani ya chumba ambacho walikuwa na akasema, ***"Amani iwe kwenu…kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi"* Yohana 20:19, 21*).*** Yesu ni amani yetu na tunapotumwa na yeye, tunapaswa kuondoka na kuhudumu amani hiyo kwa watu. Baada ya kuwatuma ***"Akawavuvia, akawaambia, pokeeni Roho Mtakatifu"* Yohana 20:22.** Roho Mtakatifu hupokelewa tunapompokea Yesu kama Amani!

***Yesu amelidhihirisha jina la "Yehova Shalomu"***

### 6) YEHOVA ROHI – "MIMI NIKO Mchungaji wako"

Ufunuo wa Yule wa milele akiwa mchungaji wetu alikuja kupitia Daudi katika **Zaburi 23:1** ambayo inasema ***"Yahweh (BWANA) ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu".*** Kwa kutupatia mahitaji yetu, kutulisha, kutushughulikia, kutuponya na kutuelekeza, yeye ndiye mchungaji wetu. Kama mchungaji, ***"hunihuisha nafsi yangu"*** (**aya 3**)**.** Palikuwa na unabii mwingi katika agano la kale ambayo inaongea habari za Mungu akiwa mchungaji na pia ikiongea habari za Yule atakaye kuja kuwachunga watu wa Mungu. Ezekieli alitabiri, ***"Na mtumishi wangu, Daudi atakuwa mfalme juu yao, nao wote watakuwa na mchungaji mmoja; nao wataeneda katika hukumu zangu na kuzishika amri zangu na kuzitenda"* Ezekieli 37:24.** Mungu alikuwa aje kama muchungaji kwa watu wake kupitia mfalme katika uzao wa Daudi. Moja wapo ya majukumu ya mchungaji ni kuongoza kondoo katika malisho bora na utulivu, ambayo unatuingiza katika urithi wetu!

### Mchungaji wetu ni nani?

Yesu alisema, ***"MIMI NIKO mchungaji mwema"* Yohana 10:11.** Yesu aliiweka wazi ya kwamba yeye ndiye utimilifu wa "Ýahweh Rohi". Pia yeye ni mlango wa kondoo na kupitia yeye tunapata malisho (**Yohana 10:9**). Yeye ndiye mfalme ambaye Ezekieli alitabiri kuhusu atakayekuwa mchungaji mmoja!

Katika **Waebrania 13:20** inasema ***"Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake".*** Yeye ndiye mchungaji mkuu ambaye anatukamilisha!

Katika kuwahimiza wazee wenzake, Petro anawaambia, kwamba wakiendelea kuwachunga kondoo wa Mungu vyema ***"Na mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka"*** **1 Petro 5:4.** Yesu ndiye Mchungaji Mkuu, udhihirisho wa jina la Mungu, ***"Yahweh Rohi",*** akituita "***njoni kwangu… jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; … nanyi mtapata raha nafsini mwenu"*** **Mathayo 11:28-29.**

***Yesu amedhihirisha jina la "Yahweh Rohi"!***

### 7) YEHOVA TSIDKENU - "MIMI NIKO Haki yenu"

Jeremiah alikuwa akitabiri juu ya kiongozi mkuu atakaye kuja kutoka kwa ukoo wa Daudi ambaye atatawala na kutenda kwa hekima, atafanya ***"hukumu na haki katika nchi. Na jina lake atakaloitwa ni hili, Yahweh (BWANA) ni haki yetu"*** **Jeremia 23:5-6.** Jina la mtawala, Masihi atakayekuja, itakuwa Mungu wa milele, "MIMI NDMI", haki yenu!

Pia katika **Yeremiah 33:15-16**, Yeremia anasema sio kwamba tu ataitwa jina hili, lakini pia Yerusalemu mji wa Mungu utaitwa kwa jina hilo, ***"Yahweh ni haki Yetu".*** Mungu wa milele ndiye haki yetu na ndiye aliye haki na amejawa na haki (**Kum 32:4).**

### Haki yetu ni nani?

Mtume Paulo anatangaza katika **1 Wakorintho 1:30** kwamba Kristo Yesu ***"Alifanyika kwetu hekima itokayo kwa Mungu…na haki"*** **Yesu Kristo ni haki Yetu!** Mtume Yohana anasema kwamba "***na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki"*** **(1Yohana 2:1).** Yesu ndiye mwenye haki na hiyo ilimwezesha kuwa, "***kiptanisho kwa dhambi zetu"*** **(1Yohana 2:2).** Kwa kuwa kipatanisho Mungu alimfanya ***"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi sote tuwe haki ya Mungu"*** **(2 Wakorintho 5: 21);** na kwa hivyo tuna utimizo, udhihirisho wa Jina, "Yahweh haki yetu". Ni jina lake na tunapokea haki yake kwa imani, tukilidhihirisha jina hilo!

Mtume Paulo anasema, ***"Ili nimpate Kristo, tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki Yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu kwa imani…"*** **(Wafilipi 3:8b-9).** Kupatikana ndani ya Kristo yamaanisha kuwa ndani yake aliye haki yetu!

***Yesu ndiye udhihirisho wa jina "Yahweh Tsidkenu"***

### 8) YAHWEH SHAMMAH – "MIMI NIKO HAPO"

Nabii Ezekieli alikua akitazama mbele kuona siku ambayo mji wa Mungu utaimarishwa na kujengwa na Hekalu ikiwa ndani. Huu sio mji wa kawaida lakini ni mji ambao Ibrahimu aliona, ***"wenye misingi***, ***ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu"*** **(Waebrania 11:10).** Ezekieli aliona kukamilika kwa mji huu, ***"Na jina la mji huo tangu siku hiyo litakua hili, BWANA YUPO HAPO"*** **(Ezekieli 48:35).** Wakati mji huo wa milele utakapokamilika, Mungu wa milele atapata pumziko katika mji huo na atapatikana hapo!

### Ni nani yuko?

Wakati Yesu alikuwa akifundisha kuhusu kufunga na kufungua kuhusu ndugu anayetenda dhambi katika kanisa, anasema kwamba, ***"Kwa kuwa walipo wawili watatu, wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao"*** **Mathayo 18:20.** Yeye

yupo! wakati wawili au watatu wako katika kupatana na kukubaliana na umoja katika jina laYesu, jina la "Yahweh Shammah" linadhihirika! **"MIMI NIKO hapo miongoni mwao!"**

Wakati Yesu alikuwa akiwaandaa wanafunzi wake kwa kuondoka kwake anawaambia kwamba atamtuma Roho wa kweli, ***"ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtabui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakua ndani yenu"*** **Yohana 14:17.** Roho wa kweli alidumu **nao** kwa njia gani? Kwa maana alikuwa amesimama mbele yao ndani ya Yesu! Tena anasema sio tu kwamba **nanyi** lakini pia atakaa **ndani** yenu! ***"Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu"*** **Yohana 14:18.** Yesu atakuwa hapo! Atakuwa ndani yako katika Roho! Yeye yuko!

## Yesu yuko katikati ya kanisa lake.

Baada ya kufufuka kwa Yesu, wanafunzi wake walikuwa wamejificha kwa nyumba pamoja ghafla, ***"Akaja Yesu, akasimama katikati…"*** **Yohana 20:19.** Katika kitabu cha **Ufunuo** Yohana anasema aliona, ***"katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu…Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai, nami nilikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele…na vile vinara ni makanisa saba"*** **Ufu 1:13, 17-18, 20.** Yesu ndiye ufunuo wa Yule Mungu wa milele katikati ya kanisa. Yeye ndiye aliyepo!

Hatimaye Yohana anasema aliona, ***"Mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu… Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakua watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao"*** **Ufu 21:2-3.** Mungu yuko kati ya mji wake, yeye yuko! Siri ya kanisa ni kwamba ni makao ya Mungu ***"katika Roho"*** **Waefeso 2:22.** Wakati kanisa linatembea katika ukomavu na ukamilifu, watu wote wataliita "Yahweh Shammah" kwa kuwa watapata kujua ya kwamba Yesu yuko pale!

***Yesu ndiye udhihirisho wa jina "Yahweh Shammah"!***

## 9) YEHOVA TSABAOTH - "MIMI NIKO wa Majeshi Yangu"

Kabla ya Waisraeli kuchukua Yeriko, Yoshua kama kiongozi wa watu aliienda kumtafuta Mungu. Walikuwa waingie katika urithi na Yoshua ilionekana alikuwa anatayarisha moyo wake kwa sehemu hiyo nyingine ya safari. ***"Ikawa hapo Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akavua macho yake na kuangalia, na tazama, mtu mume akasimama kumkabili mbele yake, naye alikuwa na upanga wazi mkononi mwake; Yoshua akamwendea, na kumwambia, Je! Wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu? Akasema, La, lakini nimekuja sasa, nili amiri wa jeshi la Yahweh (BWANA). Yushua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu aniambia nini mimi mtumishi wake?"*** **Yoshua 5:13-14.** Je tukio la ajabu namna gani. Yoshua alikutana na amiri wa Jeshi la Yahweh na akamwabudu. Kama huyu hakuwa Mungu, Yoshua hangeruhusiwa kumwabudu – hii ilikuwa ni tukio, udhihirisho wa Mungu kwa mfano wa mwanadamu aliyeamuru majeshi ya Yahweh.

Yoshua alikumbushwa ya kuwa hakuwa katika uongozi wa jeshi ambalo lilikuwa likielekea kanani, lakini jeshi ilikuwa la Yahweh na Yahweh yupo miongoni mwa jeshi lake. Akipigana Vita mwenyewe!

## Majeshi ni akina nani?

Sisi kama waamini tumekuwa na mawazo ya kiroho ya mbinguni ya maandiko yote ambayo imetupofusha kuona ukweli. Katika **Kutoka 6:26**, inasema ***"Hawa ni Haruni ye yule,***

***na Musa ye yule, Yahweh aliowaambia akisema, Watoeni wana wa Israeli watoke nchi ya Misri sawasawa na majeshi yao".*** Jina hili amiri mara kwa mara limetafsiriwa **"majeshi"** tukimweleza Mungu wa milele kama **"Yahweh (BWANA) wa majeshi".**

Katika **Kutoka 7:4** inasema ***"Lakini Farao hatawasikiza ninyi, nami nitaweka mkono wangu juu ya Misri, na kuyatoa majeshi yangu, watu wangu, hao wana wa Israeli, watoke nchi ya Misri kwa hukumu zilizo kuu".*** Kama uko na Bibli ya New King James utatambua kwamba "na" katika aya hii iko katika Italiano. Hii inamaanisha kwamba jina hii haiko katika maandiko ya kwanza ya Kiebrani lakini iliongezwa na watafsiri ili ilete maana. Hata hivyo katika hali hii na katika hali zingine unaweza kuwaona watafsiri walikuwa wakipigana na mawazo yale ambayo wengi wetu wamekuwa nayo. Tumefikiria kwamba "Majeshi" ni malaika wa mbinguni lakini ukisoma bila "na", ambayo iliongezwa, inasema "Na kuyatoa majeshi yangu, watu wangu, hao wana wa Israeli…" Hallelujah! Majeshi ni watu wa Mungu! Mungu hakuwa akikomboa malaika wa mbinguni kutoka Misri – alikuw akiwakomboa watu wake na kuwatoa kama jeshi lake!

Hii inabadirisha njia yote ambayo tumeona Jeshi. Ndio, Mungu ni Mungu wa jeshi la malaika pia, lakini katika matukio mengi anajidhihirisha kuwa Yule wa milele ambaye ameonekana katika jeshi lake, watu wake. Anajidhihirisha kwa ushindi kupitia watu wake!
Kutajwa mara ya kwanza kwa jina **"Yahweh Tsabaoth"** ni katika **1 Samweli 1:3** katika mazingira ya kumtolea sadaka kule Shiloh. Imetajwa zaidi ya mara mia mbili katika agano la kale! Yeye anajulikana kama Mungu wa majeshi yake, Mungu wa watu wake!

## Yesu amri wa majeshi!

Yoshua alimwabudu Mungu alipokuja kwa mfano wa Mwanadamu! Huyu ni Yesu! Alimwongoza Yoshua katika nchi ya ahadi na hivyo atatuongoza! ***"Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu"*** **2 Wakorintho 2:14.** Yesu anatuongoza katika ushindi; adui zetu wakishindwa! Miongoni mwa jeshi hii, harufu ya Kristo inadhihirika! Yeye ndiye aliye kati ya watu wake!

Paulo anasema kwa Timotheo, ***"Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu"*** **2 Timotheo 2:3.** Timotheo alikuwa askari katika jeshi la Yesu. Katika kitabu cha **ufunuo** Yohana anaandika, ***"Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu mwenyezi. Naye anajina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA"*** **Ufunuo 19:14-16.** Yesu anaongoza kwa ushindi kama amri wa majeshi yake. Jeshi lake limavalia kitani safi. Sio malaika kutoka mbinguni ila, ***"hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya mwana- kondoo"*** **Ufu 7:14**. Yesu analiongoza jeshi lake kutoka Misri mpaka nchi ya ahadi. Yeye ni ***"Yahweh wa Mjeshi"*** **–** Yule wa milele wa watu wake!

### *Yesu amelidhirisha jina la "Yahweh wa majeshi"*

## Ufunuo wa Yule wa milele

Katika injili ya Yohana, nyakati zimetajwa ambapo Yesu amejidhihirisha kuwa Yule wa milele. Kuna matukio nane haswa katika nakara ya Yohana ambapo Yohana anatumia msemo huu wa ajabu. "**MIMI NIKO"** kujifunua, akidhihirisha jina laMungu!

i. ***"MIMI NIKO Mkate wa uzima"*** **Yohana 6:48**
ii. ***"MIMI NIKO Nuru ya ulimwengu"*** **Yohana 8:12, 9:5**
iii. ***"MIMI NIKO Mlango"*** **Yohana 10:9**
iv. ***"MIMI NIKO I Mchungaji mwema"*** **Yohana 10:11**
v. ***"MIMI NIKO I Ufufuo na uzima"*** **Yohana 11:25**
vi. ***"MIMI NIKO I Njia, kweli na Uzima"*** **Yohana 14:6**
vii. ***"MIMI NIKO I Mzabibu wa kweli"*** **Yohana 15:1**
viii. ***"Amin, amin, nawaambia, kabla Ibrahimu hajakuwako, MIMI NIKO" Yohana 8:58.***

Tukio la **nane** ndio iliyo wazi kabisa. Yesu alikuwa akiongea na Mafarisayo na hawangemuelewa alipo sema Alimjua Ibrahimu. Walisema ***"Wewe hujapata bado miaka hamsini, nawe umemwona Ibrahimu? Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, kabla Ibrahimu hajakuwako, MIMI NIKO"*** **(Yohana 8:57-58).**

Jina la Mungu wa milele katika agano la kale lilimfunua kama **"MIMI NIKO".** Yesu alikuwa udhihirisho wa jina hilo katika mtu! Yule wa Mungu milele alifanywa mwili! **Yesu ndiye "MIMI NIKO"!** ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo"*** **Mdo 4:12.**

Yesu alisema, ***"Nimelidhihirisha jina lako kwa wale ulionipa".*** Yesu, kupitia maisha yake na kuwepo, alilifunua jina la Mungu kwa watu. Jina la Mungu lilifunuliwa ndani ya **Yesu!**

### YESU NDIYE UDHIHIRISHO WA JINA LA MUNGU!

# KUOSHWA KATIKA UTUME

## Ufunuo wa Mwana wa Mungu – Yohana 9

### Yesu alimwona mtu kipofu tangu kuzaliwa.

**Aya 1** katika **Yohana 9:1** mtume Yohana anaandika, ***"Hata alipokuwa akipita alimwona mtu kipofu tangu kuzaliwa".*** Mtu huyu alikuwa Myahudi; alikuwa mmoja wa watu wa Mungu, katika "kanisa" lasiku zake. Twasoma baadaye katika hadithi hii kwamba viongozi wa dini ya Kiyahudi, Wafarisayo, walimchukua mtu huyu kumhoji, ambayo inaonyesha kwamba alikuwa sehemu ya dini yao.

Mtu huyu alikuwa ni wa jamii ya Mungu lakini alikuwa na shinda – alikuwa kipofu na alikuwa kipofu tangu **kuzaliwa**! Inawezekana kuzaliwa tena na kuwa sehemu ya kanisa, sehemu ya jamii ya Mungu na uwe kipofu - kipofu katika mapenzi na kusudi la Mungu. Kote katika kanisa la ulimwengu kuna waamini waliookoka ambao wamezaliwa upya katika dini au miundo ambayo hairuhusu ufunuo mpya wa neno laMungu kuwabadilisha. Wanakwama katika mahali padini isiobaduka na kubadirishwa na ufunuo ambao unakuja kutoka kwa enzi ya Mungu kwa watu wake.

Twahitaji **kufunguliwa macho yetu! Yesu alimtambua mtu huyu** .

### Wanafunzi wanatafuta suluhu

**Aya 2** katika **aya 2**, inasema, ***"Wanafunzi wake wakamuuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?"*** Wengi wetu leo hii wanatafuta ni kwa nini tuko katika hali fulani, kwa nini tuna baathi ya matatizo – pengine baba zetu walitenda kitu kibaya na diposa tunalipa dhambi zao. Wanafunzi, kama sisi, walikuwa wakiangalia kiini na kwa kuyatenda hayo ikaadhiri uwezo wao wa kuwa na uhusiano na Mungu, walikuwa wanakosa mpango na moyo wa Mungu.

**Aya 3** ***"Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mugu zidhihirishwe ndani yake".*** Jawabu ya Yesu ilikuwa nyepesi. Yeye sio mzito. Aliwaambia wanafunzi wake waache kutafuta shida na wafahamu Mungu alitaka mtu huyu aponywe! Mungu alitaka arejeshwe, alitaka kazi zake zidhihirishwe katika maisha yake! Yesu hakuja kuwa mtazamaji na kuchunguza shinda za ulimwengu – alikuja kutuokoa kutukomboa na kuturejeshea kuona kwetu! Hebu tupokee moyo huu ndani yetu ili tutembee na Mungu katika njia ambayo tutaona vile anafanya mpango wake katika maisha yetu ya kila siku.

### Kuzifanya kazi zake aliyetutuma

**Aya 4** ***"Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana; usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi".*** Baada ya kuwaambia Mungu alitaka kufanya kazi ndani ya mtu huyu, kisha akasema ni lazima azifanye kazi zake **aliyemtuma**. Neno la ***"kutuma"*** ni neno la Kiyunani **"apostello"** ambapo tunapata neno la kingereza "**mtume".** Yesu kama mtume wa Mungu **alitumwa** kufanya kazi na Baba. Tunapaswa kufanya ambacho tumetumwa kufanya. Kuna waamini wengi kote ulimwenguni ambao wanajaribu kueneda na kufanya kazi ya Mungu bila **kutumwa.** Twahitaji kutumwa. Tunapotumwa tuko katika mapenzi ya Mungu na tuna mamlaka kutenda mapenzi ya Mungu katika maeneo tumetumwa.

### Yesu aliwatuma mitume wake

Katika **Mathayo 10** Yesu aliwatuma mitume wake kuzifanya kazi katika Miji ya Israeli. Maandiko yanasema, ***"Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Na katika kueneda kwenu, hubirini mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure toeni bure"*** **aya 5-8.** Mitume walitumwa kuzifanya kazi za Mungu na walikuwa na mamlaka kufanya katika maeneo waliotumwa ambayo Yesu aliwapatia. Kama wangeenda mahali pengine kujaribu kufanya ambacho Yesu alisema, hawangekuwa na mamlaka ya kufanya hayo, na pengine wangemalizia kama wana wale saba wa Skewa katika **Mdo 19:13-16.**

### Tunahitaji kujua yule ambaye ametutuma!

Wakati tunaeneda na mamlaka ya Kristo ambaye ametutuma, tuna mamlaka yake kuyatenda ambayo ametuagiza. Kuna Wakristo wengi waasi duniani ambao hawajinyenyekeshi ili kutumwa. Waliondoka kumfanyia Bwana kazi lakini wanataka kufanya mambo kwa njia yao. Yesu alisema. ***"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbiguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!"*** **Mathayo 7:21-23.**

Yesu alisema ni lazima **azifanye kazi za Yule aliyemtuma!** Twahitaji vivyo hivyo; angalia kile ambacho Baba yetu anafanya na ukifanye (**Yohana 5:19**). Mungu anataka kipofu aone! anataka watu wake wakomae katika maarifa ya ufunuo wa Mwana wa Mungu (**Efe 4:13)**.

### Nuru ya ulimwengu

**Yohana 9:5** ***"Muda nilipo ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu".*** Yesu alimwona kipofu na jawabu yake ilikuwa, ***Mimi ndiye nuru ya ulimwengu!*** Yesu ndiye nuru tunayohitaji. ***"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho wa Mungu akatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema Iwe nuru; ikawa nuru"*** **Mwazo 1:1-3.** Katika giza ya ulimwengu huu Mungu aliachilia nuru; alituma nuru! Ilikuwa haina umbo, tupu na giza na jambo la kwanza Mungu alitaka kufanya ni kuachilia nuru! Nuru hii ilikuwa ni ufunuo. Ilikuwa ni hekima, ufahamu, na maarifa ikiachiliwa ulimwenguni kufunua jinsi ya kujenga, jinsi ya kuimarisha na jinsi ya kujaza **(Mithali 24:3-4**). Baada ya nuru kupeanwa, viumbe vilirejeshwa!

***"Hapo mwanzo kulikuweko Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza"*** **Yohana 1:1-5.** Neno ni nuru. Ni uzima na giza haiwezi kuitambia. Nuru ni ufunuo wa Yesu. Yesu alimwona mtu huyo mmoja wa watu wake, na alikuwa kipofu; kipofu kwa mambo ya Mungu, kipofu kwa kusudi lake, ukuu na upendo. Yesu alisema kwamba ***"Muda nilipo ulimweguni, mimi ni nuru ya ulimwengu".*** Ulikuwa wakati wa kufunua nuru kwa ndugu huyu kipofu na kumwona akirejeshwa!

### Kupakwa lakini bado kipofu

**Yohana 9:6** ***"Alipokwisha kusema hayo, alitema mate chini, akafanya tope kwa yale mate. Akampaka kipofu tope za macho".*** Baada ya kazaliwa mara ya pili, ambayo inahusisha kubatizwa ndani ya mwili **(1 Wakorintho 12:13**), twahitaji kubatizwa na Roho Mtakatifu. Twahitaji kubatizwa ndani ya Roho kuachilia nguvu zetu za kushuhudia (**Mdo 1:8**). Hata hivyo, upako ijapokua unaachilia nguvu, karama na uwezo wa kufanya kazi, haiachilii ufunuo kamili ambao tunahitaji. Kumbuka wale watu wote ambao wanafanya kazi zote lakini ni waasi. Mtu huyu sasa alikuwa amepakwa lakini alikuwa **haoni**! Yesu anataka kufungua kuona kwetu.

Ujuzi wa pentekote sio mwisho. Ni ya muhimu kwetu; ndiposa Yesu alimpaka mtu huyu. Ujuzi wa kipentekote haswa haufungui macho yetu kwa kusudi la milele. Inatupatia imani na uhakika na ni hakikisho ya urithi wetu (**Efe 1:13**). Hata hivyo, mtu huyu alikua akitembea katika ulimwengu wa giza. Kanisa la pentekote kwa sehemu kubwa wanatembea katika giza. Tumepakwa na mambo mengi ya nguvu yanaendelea kufanywa lakini ni wakati wakuona utimilifu wa Mungu ukifunuliwa!

### Nenda kanawe katika birika ya Siloamu

**Yohana 9:7** ***"Akamwambia, nenda kanawe katika birika ya Siloamu, (Maana yake, aliyetumwa). Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona".*** Baada ya Yesu kumpaka mtu huyu, alimwambia akanawe katika birika ya **"kutumwa"**, kisima cha '**apostelo**' birika ya utume! Ilikuwa tu ni baada ya kuoga katika birika hii ***"Alirudi anaona"*** Hallelujah! Tuko katika siku za urejesho wa kiutume - kuja katika msingi wa kitume ambayo Yesu aliweka kanisa na kuna ufunuo mkubwa!

Baathi ya watu wanaweza kusema kwamba hii ni kuhofisha sana kutilia maanani utumiaji wa jina hili **"Tuma"**. Hata hivyo, kuna mara nne tu katika uandishi wa Yohana ambapo anatuambia utafsiri wa maneno kutoka Kiebrania kwa Kiyunani. Anatafsiri **"Rabi"** kuwa **"Mwalimu" (Yohana 1:38);** anatafsiri jina **"Masihi"** kuwa **"Kristo" Yohana 1:41,** anatafsiki **"Kefa"** kuwa "**Jiwe" Yohana 1:42;** na kisha anatafsiri jina "**Siloamu"** kuwa "**kutumwa".** Kawaida Roho Mtakatifu aliwaza ni ya muhimu kwetu kujua – twahitaji kutilia maanani kwa kuwa pana nufunuo wetu.

Twahitaji kunawa katika birika ya **"Kutumwa"!** Itakubadirisha; utapata kuona! sio kipofu tena! Utakuja katika ufunuo wa siri, ***"Ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake"*** **Wakolosai 1:26.** Kuna birika ya kitume ambayo tunaweza kunawa ndani yake. Ni Yesu, ***"alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"*** **Waefeso 5:26-27.** Ni kwa neno la Bwana ambapo tunaoshwa! Yesu alisema, ***"Nenda kanawe katika birika ya Siloamu (ambayo imetafsiriwa, kutumwa)".*** Yesu anatuambia tuwe watu wa kitume; watu ambao wemetumwa. Tunalo neno likidumu ndani yetu na kwa hivyo tuna mamlaka. Lakini tunapaswa kunawa kwanza ili macho yetu yapate kufunguliwa!

### Ufunuo wa kitume – kuuweka mwili katika mpangilio

Baada ya kunawa katika birika bii aliponywa na akarejeshwa. Kuja katika ufunuo wa kitume inatuweka katika mpangilio. Katika **Waefeso 4:12** Paulo anaandika kwamba Yesu amepeana huduma tano kusudi la, ***"kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke,***

***hata mwili wa kristo ujengwe".*** Neno ***"Kukamilisha"*** katika lugha ya Kiyunani ilimaanisha kulainisha mfupa uliovunjika katika upasuaji. Inamaanisha "kufanya sawa, kuandaa, kufunza, kukamilisha, kutengeneza kikamilifu ili itumike,"

Huduma ya utume kama huduma ya msingi miongoni mwa tano inakuja kunyoosha mifupa ya mwili katika mpangilio. Yesu alimrejeshea huyu mtu kuona kwake ili aje pahali pake. Kunawa katika ufunuo wa kiutume itakufaidi kuona jinsi Mungu anaijenga nyumba yake, ambayo ni kanisa lake, ambayo ni mwili wake, ***"Ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"*** **Efe 1:23.**

### Kuwa na ushuhuda – kulibeba jina la Yesu

**Yohana 9:8** Sasa huyu mtu alikuwa na ushuhuda wa Kristo katika maisha yake. Waliomjua walipomwona walitatanikiwa, ***"basi jirani zake, na wale waliomwona zamani kuwa ni mwombaji, wakasema, Je! huyu siye Yule aliyekuwa akiketi na kuomba?".*** Walimjua mtu huyu kama mwombaji. Lakini ghafla alikuwa haombi tena. Kuna waombaji wengi kanisani leo. Wako katika kila mwaliko "kupokea upako zaidi", "kupokea uponyaji". Sio vibaya kueneda katika mialiko lakini ikiwa ndiyo tabia yako na njia yako ya kuhusiana na Mungu kuna shinda kubwa. Watu hawa hawajafunzwa kutembea na Yesu na kwa hivyo kila mara wanatafuta mtu wa kuwaombea. Hii sio mzuri. Ni neno linaloponya na kurejesha (**Zaburi 107:20**) – sio watu nwenye nguvu. Twahitaji kutoka katika hali ya kuwa waombaji na kupokea ushuhuda wa Yesu katika maisha yetu.

Waliomtambua mtu huyu walishangaa. Mara alikuwa akitembea bila kuelekezwa na mwanadamu yeyoye – anaweza kujionea vyema yeye mwenyewe. Anajifundisha kutembea katika **nuru ya ulimwengu, Yesu.** Ana ujasiri na mamlaka ambayo haikuweko mwanzo - alikuwa amenawa katika birika ya **utume!**

**Aya 10** ***"Basi wakamwambia, macho yako yalifumbuliwaje?".*** Walitaka kujua ni kwa nini amebadirika. Tunapokuja katika ufunuo wa kitume basi tutabadirika na marafiki zetu wa dini watataka kujua ni nini kimetendeka. **Unaonaje ufunuo wa neno la Mungu sasa? Mbona unafurahia Biblia? Mbona unasema kwamba unaweza kuona mpango wa Mungu sasa?** Watataka kujua kwa sababu mara hutoshei katika hali zao tena. Uko nje ya saduku waliokuweka ndani na wanaona uhuru ndani yako wanaotaka kujua.

**Aya 11** ***"Yeye akajibu, mtu Yule aitwaye Yesu alifanya tope, akanipaka macho akaniambia, Nenda Siloamu ukanawe; basi nikaenda na kunawa, nikapata kuona".*** Ushuhuda wake haukuwa wa taratibu za dini yake, na jinsi mnenaji alivyokuwa mwisho wa juma. Alishuhudia juu ya Mtu aliyeitwa **Yesu!** Sasa akaanza kulichukua jina la **Yesu!** Kunawa katika Siloamu ni kutoka kwa dini, dhehebu, idara na kuja katika ushuhuda wa Yesu! Kuitwa kwa jina lake – kujiitanisha na yeye!

## Kulichukuwa jina la Yesu

### Mtume Paulo alilichukua jina laYesu

Baada ya Paulo kuupokea ufunuo wa Yesu, Yesu alimwambia mwanafunzi Anania kuhusu Paulo kwamba ***"Huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue jina langu mbele ya mataifa na wafalme, na wana wa Israeli"*** **Mdo 9:15.** Watu wa kitume, ambao wamenawa katika birika ya utume wanaweza kuona na watalichukua jina la Yesu. Kanisa sio la mtu! Kanisa halijaitwa kwa jina la dini yenu! Kanisa katika maandiko limeitwa kwa jina la Yesu! Yesu

alisema, ***"Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamnipokei; mwingine akija kwa jina lake mwenyewe mtampokea huyo"*** **Yohana 5:43.** Twahitaji kuitanishwa na Yesu na sio kuwa na kujipatiana kwa wanadamu kusikostahili!

Yesu alimwakilisha yeye **aliyemtuma!** Yesu alikuwa na ufunuo wa kitume! Yesu alisema ***"Yeye ampokeaye mtu ye yote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka"*** **Yohana 13:20.** Yesu alimwakilisha Baba kikamilifu na twahitajika kumwakilisha Yesu, Baba yetu. Enenda ukanawe katika birika ya **aliyetumwa!** Lichukue jina la Yesu. Tumwa na Yesu na mitume aliowatuma. Ukiwapokea mitume aliowatuma unampokea! Hallelujah! Huu ni ufunuo wa kitume!

## Utateswa.

**Yohana 9:13-14** ***"Basi wakampeleka kwa Mafarisayo yule aliyekuwa kipofu zamani. Nayo ilikuwa sabato, hapo Yesu alipofanya zile tope na kumfumbua macho".*** Mafarisayo walikuwa ndio viongozi wa kidini wa taifa la Wayahudi. Walikuwa viongozi wa kanisa na mojawapo wa taratibu zao ziliharibiwa na Yesu. Yesu alikuwa na tabia ya kufanya mambo ya ajabu siku ya sabato. Hakika hili liliwafanya Mafarisayo kukasirika kwa maana iliendelea kutatiza watu katika mikutano yao ya kanisa. Mafarisayo hawakuwa na ufunuo wa sabato. Walikuwa wamefungwa na dini, kazi na mambo ya utamaduni wa mwanadamu ambayo iliwazuia kuona kwamba Yesu alikuwa ameleta kutimiza yale yote ambayo yaliwakilishwa na sabato.

Sabato ilikuwa ni kuingia katika pumziko ya Mungu! Kutimizwa kwa sabato ni kuingia katika pumziko la Mungu la milele, kuingia katika utimilifu wa ahadi za mungu na kupata pumziko ndani yake. Mwandisi wa **Waebrania** anasema, ***"Basi inasalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake"*** **Waebrania 4:9-10.** Yesu alikuwa akiwaleta watu katika urithi huu. Katika siku ya sabato Yesu alifanya miujiza mingi ambayo iliwatoa watu katika utumwa na katika kuwaleta katika pumziko. Alikuwa akitimiza sabato kama walikuwa na macho ya kuona.

**Aya 17** Sasa mtu huyu aliletwa mbele ya viongozi wa dini ili ahojiwe juu ya uponyaji wake. Wakati mwondoko wa Mungu unafanyika huwa kuna wale hawataelewa na watapingana na Mungu kwa sababu haikufanyika vile walidhani – kulingana na taratibu zao. **Lakini hii ilifanyika nafasi ya mtu huyu kumshuhudia Yesu!** Wakati Mafarisayo waliongea kuhusu waliyemdhania Yesu kuwa, wakifikiria alikuwa mtenda dhambi kwa kufanya uponyaji siku ya sabato, wakamuuliza mtu ambaye mwanzo alikuwa kipofu jinsi anavyosema kumhusu Yesu. Jawabu yake ilikuwa ***"Ni nabiii"*** **Yohana 9:17**. Huo ulikuwa ni ufunuo mwema lakini Mungu alitaka kumpeleka ndani zaidi!

## Ujuzi ni mkubwa kuliko muundo

Usishangae wakati macho yako yanafumbuka katika uhakika wa Mungu – kwa nuru ya ulimwengu – ambapo walio katika mamlaka ya udini watasimama kinyume chako na kukuhoji. ***"Jihadhalini na wanadamu; kwa maana watawapeleka mabarazani, na katika masinagogi yao watawapiga… lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri – fikiri jinsi mtakavyosema, maana matapewa saa ile mtakayosema"*** **Mathayo 10:17, 19.**

**Yohana 9:24-25** Ujuzi ni kubwa kuliko muundo! Baada ya kuwauliza wazazi wake kudhibitisha uhakika wa upofu wake tangu kuzaliwa wakamuuliza yule mtu tena, ***"Mpe Mungu utukufu. Sisi tunajua yakuwa mtu huyo ni mwenye dhambi. Basi Yule mtu akajibu, Kwamba yeye ni mwenye dhambi sijui. Najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sasa naona".*** Wakati unapata ufunuo hauwezi saidia ila tu kushuhudia. Hauwezi kusaidia ila tu kuongea ukweli! Shahidi ni mtu ambaye amepitia jambo kwa uhakika kwa kugusa, kuonja, kuona, kusikia ama kunusa. Mungu ni wa kweli! Wakati anapofumbua macho yako imetendeka – hakuna kuangalia nyuma au kukana! Mungu anawainua mashahidi wa kweli duniani ambao wameoshwa katika birika ya kitume!

### Utarushwa nje

**Yohana 9:27** Baada yaMafarisayo kumsikia akishuhudia akawauliza kama walitaka kufanyika wanafunzi wake. Wakaanza kuongea juu ya kuwa wanafunzi wa mtu aliye kufa – wanafunzi wa Musa. Ni mara ngapi tunapenda kuweka tamaduni juu ya mtu. Kuna madhehebu mengi sasa ambayo yamewekwa kwa watu wa Mungu siku zilizo pita. Baadhi ya watu hawa walikuwa wakuu, lakini ukuu wao haukuwa ndani yao – ilikuwa ni ndani ya Yule alifanya kupita hao. Yesu alikuwa amesema hapo mwanzo, ***"Msidhani kwamba mimi nitawashitaki kwa Baba; yuko anayewashitaki, ndiye Musa, mnayemtumaini ninyi. Kwa maana kama mngalimwamini musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu"*** **Yohana 5:45-46.** Hapakuwa na wokovu ndani ya Musa lakini palikuwa na wokovu ndani ya Yule Musa alimtazama! Usiwafuate wanadamu – mfuata yule ambaye anawapa wanadamu mamlaka yao!

**Aya 32-34** Mafarisayo walibishana kwamba Yesu hakuwa wa Mungu kwa kuwa hawakujua alikua ametoka wapi. Mtu aliyekuwa kipofu mwanzo alisema, ***"Tokea hapo haijasikiwa ya kuwa mtu ameyafumbua macho ya kipofu, ambaye alizaliwa hali hiyo. Kama huyo asingalitoka kwa Mungu, asingeweza kutenda neno lo lote. Wakajibu, wakamwambia, Ama! wewe ulizaliwa katika dhambi tupu, nawe unatufundisha sisi? Wakamtoa nje"*** Wakati hatuwezi kuubeba ufunuo wakati mwingine inatufanya tuwe hatuna usalama na tunataka kuutupilia mbali. Hivyo ndivyo watu walifanya kwa huyu mtu aliyekuwa kipofu kwanza. Nje ya kanisa! Hakuwa tena sehemu ya ibada ya Wayahudi; alifukuzwa nje ya muundo wao. Hallelujah! Hapa ni mahali pazuri pa kuwa! Aliyabeba majaribu, mateso. Hakukana alichokijua. Alidhibitisha mwaminifu na hii ni ya kumpendeza Mungu.

Wengi ambao wamekuja katika ufunuo wa kiutume wameyapitia mambo yale kupiti kwa dini zao na miundo ya kanisa zao. Wengi husema, ***"Lakini hatujui wametoka wapi. Tunaweka utamaduni wa Jonn Wesley au Martin Luther au yeyote yule".*** Wandugu ni wakati wa kutoka kwenye vifungo na kukamatwa na udini. ***"Nikamwita mwanangu atoke Misri"*** **Hosea 11:1.** Kutoka kwa kutatanikiwa, ambako kunatufunga na kutuweka kwa kufikiri katika mazingira ambayo hairuhusu ufunuo. Mtu huyu sasa aliitwa kutoka ulimwenguni na Mungu alikuwa na jambo la kumwonyesha!

## Ufunuo wa Yesu, Mwana wa Mungu.

### Ishara ya ukomavu.

Moja wapo wa ishara ambayo kanisa linakuja katika ukomavu ni ***"Hata na sisi sote tutakapo ufikia… kumfahamu sana Mwana wa Mungu"*** **(Waefeso 4:13).** Mtu huyu alikuwa na ujuzi na Yesu; alikuwa amepokea kuona kwake na sasa alikuwa hajafungwa kwa miundo ya

dini. Hii ilimletea mateso na kukataliwa lakini alishinda jaribio. Hakukana uhakika wa yale yaliyotendeka lakini alibaki mwaminifu kushuhudia juu ya ukweli.

**Yohana 9:35** Wakati haya yalitendeka, ***"Yesu akasikia ya kwamba wamemtoa nje".*** Unahitaji kujua wanapokutesa, kukuingilia na kukurusha nje Yesu huyasikia! Yesu alikuwa akifuatilia matukio – akiona jinsi huyu mtu ataendelea katika jaribio hili. Yesu anatutambua na hakuna jambo ambalo linampita. Twatakiwa kukaa waaminifu na Yesu atasikia!
Baada ya kuyasikia ***"Naye alipomwona…"*** **Yohana 9:35b,** Yesu atakuja na akupate. Wakati utapokea ufunuo wa kiutume, hautatoshea katika miundo; unaweza kurushwa nje; lakini hii inastahili kukufariji. Jambo la kwanza linalotendeka ni kwamba Yesu anakuja na kukupata! Wewe unapatana na Yesu! Unapatana naye ***"Nje ya kambi, tukichukua shutumu lake"*** (**Waebrania 13:13**). Anakuja kwako na kusongea pamoja nawe kwa maana anataka upokee ufunuo wa yeye ni nani. Mtu huyu kama Wayahudi wa kidini wa siku zake, walikuwa na mtazamo wa yule waliofikiria Masihi angekuwa. Lakini Yesu hatoshei katika viwango na maelezo ya mwanadamu. **Yeye ndiye! Ndiye aliye alicho na atakuwa atakachokuwa**! Yeye huja kwa njia ya ufunuo!

## Unaamini katika Mwana wa Mungu?

Wakati Yesu alifika kwa huyu mtu alimuuliza, ***"Wewe wamwamini Mwana wa Mungu?"*** **Yohana 9:35.** Swali la ajabu jinsi gani! Ni vyema tumruhusu Yesu kutuuliza swali hii. Ukijibu kwa ufunuo utabarikiwa milele. Macho yako yakifumbuliwa kwa uhakika wa swali hili, utabadirishwa daima! **Unamwamini Mwana wa Mungu?** Ni kwa nini Yesu aliuliza swali hii? Ni kwa nini hakumuuliza kama anamwamini Kristo, lakini, ***"Mwaonaje katika habari za Kristo? Ni Mwana wa nani? Wakamwambia, ni mwana wa Daudi. Akawauliza, Imekuwaje basi Daudi katika Roho kumwita Bwana, akisema, Bwana alimwambia Bwna wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako? Basi, Daudi akimwita Bwana, amekuaje ni mwanawe? Wala hakuweza mtu kumjibu neno; wala hakuthubutu mtu ye yote tangu siku ile kumuuliza neno tena…"*** **Mathayo 22:42-45.** Watu wa dini wa siku zile hawakuwa na shinda na kuja kwa Kristo kama vile wakristo wengi leo hawana shinda na kuelewa kuja kwa Kristo. Lakini ni Mwana wa nani?

Hili linatatiza. Ulimwenguni kote ni tatizo kanisani kwamba wengi hawafahamu Yeye ni nani. Wakati Saulo (Paulo) alipata ufunuo wa Yesu katika njia na vile alipokea Roho na kubatizwa yasemekana kwamba, ***"Mara akahubiri Yesu katika masinagogi, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, Na wote waliosikia wakashangaa…"*** **(Mdo 9:20-21).** Sauli alipokea ufunuo ambao ulimbadirisha. Alidhani kwamba alimjua Mungu lakini wakati alipatana na Mungu, alisema***, "U nani wewe Bwana?" Naye akasema, "Mimi ndimi Yesu …"*** (**Mdo 9:5**). Akapata ufunuo wa Mwana wa Mungu.

## Mwana ni sawa na Baba

**"*Basi kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivuja sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba Yake, akijifanya sawa na Mungu"*** **Yohana 5:18.** Hii ndio siri. Ni: ***"Siri ya Mungu, yaani Kristo…"*** **(Wakolosai 2:2).** Siri ni ipi? Ni: ***"Mimi na Baba tu umoja"*** **Yohana 10:30.** Ni siri ya utaua, kwamba ***"Mungu alidhihirishwa katika mwili…"*** (**1Timotheo 3:16**). Kuwa Mwana wa Mungu haimaanishi kwamba Mungu alikuwa na mtoto, inamaanisha kwamba Mungu alifanyika mwanadamu!

## Mwana wa Mungu ni Mungu katika mwili!

Yesu alisema kwa mtu huyo, ***"Unamwamini Mwana wa Mungu?"*** Yesu alikuwa akimuuliza kama aliamini Mungu angefanyika mwanadamu. Alikuwa akiuliza mtu huyo kama aliamini kwamba Mungu angejionyesha na ajifunue kwake kikamilifu ndani ya mtu. Alikuwa akimuuliza kama aliamini kwamba Mungu yuko duniani!

## Yesu ni Mungu akifunuliwa

**Yohana 9:36-37** ***"Naye akajibu akasema, Ni nani, Bwana, nipate kumwamini? Yesu akamwambia, Umemwona, naye anayesema nawe ndiye".*** Ho! Jawabu gani! Yule mtu aliamini lakini alitaka maelezo. Yesu alimpa. **Umemwona na ndiye anaongea na wewe!** Sio tu kwamba macho yake yalifumbuliwa kiasiri – yalifumbuliwa kiroho kumwona mwana wa Mungu! Alipata ufunuo wa Mwana wa Mungu!

## Alimwabudu yeye

**Yohana 9:38 "*Akasema, Naamini, Bwana. Akamsujudia".***

***AKAMSUJUDIA!*** haumsujudii mwanadamu! unamsujudia Mungu pekee! Wakati Yesu alijaribiwa na shetani nyikani, shetani alijaribu kumuuliza amsujudie, lakini Yesu akanukuu kutoka **Kum 6:13,** ***"Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake'"*** (**Mathayo 4:10**). Mtu huyu alipokea ufunuo! Yesu ni Mungu!

## Kuona mbele ya pazia

Huyu mtu aliona mbele ya pazia! Mwandishi wa **Waebrania** alisema sasa ***"Kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile iliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani mwili wake"*** **Ebr 10:19-20.** Huyu mtu aliona zaidi ya mwanadamu, na nje ya yale yalioonekana; akaona zaidi kupita mfano wa mwanadamuna akaona kwamba ***"Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake…"*** (**2 Wakorintho 5:19**). Mtu huyu alimwona Mungu na akamsujudia. Alimwona Mungu namna gani – alimwona Mungu katika Kristo! Alimwona Mungu ndani ya Yesu!

Hakuna ufunuo wa Mungu nje ya Yesu. Yesu ndiye ufunuo wa Mungu ***"Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili, Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka"*** **Wakolosai 2:5:9-10.** Mtu huyu alikamilishwa katika ufunuo wa Mwana wa Mungu! aliuona utimilifu wa Mungu ndani ya Yesu!

Ni wakati wetu kuingia ndani mbele ya pazia. ***"Hata imekuwa, sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili. Ingawa sisi tumemtambua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena"*** **2 Wakorintho 5:16.**

## Ni wakati wa kumwona Yesu kama alivyo!

- Sio kama mafundisho ya kidini tunafuata
- Au maungamo ya imani tunaamini
- Lakini kama Mungu wa kweli na aliye hai aliyefanyika mwili!
- Yeye ni Mwana wa Mungu – Mungu aliyefunuliwa katika mfano wa mwanadamu!
- Ni wakati wa kutazama mbele ya mwili wa Yesu na kuona mbele ya pazia,
- Kuupokea ufunuo wa Mungu ndani ya Kristo!

- "***Kumwabudu Bwana kwa uzuri wa utakatifu"***
- ***"Niutazame uzuri wa BWANA, na kutafakari hekaluni mwake"*** (**Zaburi 29:2, 27:4b**)

Petro alisema kwamba yeye ***"alikuwa ameuona wenyewe utukufu wake. Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu, huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye"*** **2 Petro 1:16-17.**

Tunapo nawa katika birika ya kitume, tunatoka kwa mambo yaliokufa ya kidini kuwa na ***"Macho ya mioyo yetu yakitiwa nuru"*** **Waefeso 1:18,** na kuja katika ufunuo ulio hai wa kumjua Yesu kama Mwana wa Mungu!

***"Ni nani ashindaye ulimwengu, ila yule anayeamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu?"*** Wakati tunaingia katika ufunuo huu tunakuwa washindi, hata ***"Mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu"*** **(Efe 3:19).**

Tunafanywa ***"kutimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka"*** (**Wakolosai 2:10**). Mamlaka inatiririka kutoka yule anayejua na kuamini katika jina la Mwana wa Mungu (**1Yohana 5:13**).

***"Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo".***

*HUYU NDIYE MUNGU WA KWELI, NA UZIMA WA MILELE"*

**1 Yohana 5:20**